NDOA NI MFULULIZO WA HUDUMA

# MSINGI IMARA

## KITABU CHA KUJIFUNZIA

## JUZUU 1

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina. (Mathayo 28: 19-20)

FDM
.WORLD

Craig Caster

*Strong Foundation* in Swahili
Marriage Is a Ministry series, Volume 1 of 5

*Msingi Imara ni Juzuu ya 1 katika Kitabu cha Ndoa ni Mfululizo wa Huduma*

**Juzuu nyingine katika Kitabu cha Ndoa ni Mfululizo wa Huduma ni:**

*Upendo ni Nini*? (juzuu ya 2)
*Mahitaji ya Kipekee* (juzuu ya 3)
*Utimilifu wa Kimwili* (juzuu ya 4)
*Uongozi wa Kimungu* (juzuu ya 5)
Mwongozo wa Kiongozi

**Vitabu vingine vya kujifunzia kutoka *FDM.word ni:***

*Msingi wa kweli kwa Mkristo: Kitabu chenye Msingi Imara kwa Mwanafunzi* na Craig Caster
*Malezi ni mfululizo wa Huduma* ya Craig Caster
*Kuwaelewa Vijana* na Craig Caster

Vitabu vyote vya kujifunzia kutoka FDM.world vinapendekezwa kwa matumizi ya masomo binafsi, katika vikundi vidogo vidogo kama nyezo za kujifunzia, pamoja na kutolea ushauri na saha.

Tafadhali kumbuka: Kurasa zote tupu kutoka kwenye nakala halisi zimeondolewa. Kwa sababu hiyo, baadhi ya namba za kurasa zinaweza kurukwa.

# Msingi Imara

Ndoa ni Mfululizo wa Huduma

Juzuu 1

Craig Caster

Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina (Mathayo 28:19-20)

Simu: (619) 590-1901
Barua pepe: info@FDM.world
Tovuti: www.FDM.world

Kitabu cha *Msingi Imara*, *Ndoa ni Mfululizo wa Huduma juzuu 1*, na Craig Caster ISBN 978-1-7331045-0-0
Hakimiliki ya toleo la Kuchapisha na Kielektroniki © 2021 na Craig Caster.
Haki zote zimehifadhiwa, marekebisho 09012020.

Isipokuwa itakaporekebishwa vingine, lakini kwa sasa nukuu zote za Maandiko zametolewa katika Biblia ya Swahili Union Version (SUV). Hatimiliki © Chama cha Biblia cha Kenya na Chama cha Biblia cha Tanzania (1997), Maandiko yote yametumika kwa ruhusa maalumu na haki zote zimehifadhiwa.

Pasipo ukomo wowote, si ruhusa kunakili, kuchapa au kuandika upya chapisho hili au sehemu ya chapisho (kwa mfumo wa e-book) au namna nyingine yoyote inayoweza kutengenezwa, kutunzwa au kutambulishwa kwenye mfumo wa upatikanaji tena, au kusambazwa; kwa umbo au kwa namna yoyote (kielektroniki, mekanikia, fotokopi, kurekodi, au vinginevyo), bila ruhusa toka katika hatimiliki zilitajwa hapo juu.

## Yaliyomo

Dibaji ....................................................................vii

Utangulizi ..............................................................ix

Somo la 1: Safari Binafsi........................................ 1

Somo la 2: Hapo Mwanzo ...................................... 7

Somo la 3: Mungu, Muumbaji wa Ndoa………. 15

Somo la 4: Dhumuni la Mungu katika Ndoa..........21

Somo la 5: Kukubaliana na Nidhamu ya Mungu ...29

Somo la 6: Msingi Imara .......................................37

Somo la 7: Vipengele Vitatu Muhimu……………43

Somo la 8: Mungu Anahitaji Upendo wako ...........51

Somo la 9: Jiwe Kuu la Pembeni............................59

Somo la 10: Mabadiliko ya Kushangaza ................67

Viambatanisho .......................................................75

Maelezo ya Mwisho................................................91

Kuhusu Mwandishi………………………………93

Kuhusu Huduma ya Uanafunzi katika Familia.......95

## Dibaji

Mungu aliumba taasisi tunayoiita ndoa na leo hii iko chini ya shambulio kali. Kauli hiyo inaweza kusikika kama ya kushangaza kwako, lakini athari mbaya zaidi hutoka ndani ya uhusiano kati ya mume na mke. Baada ya wanandoa kuoana, kila mmmoja huanza kuvutia kwake kulingana na mahitaji na matakwa yake. Kadri muda unavyopita, matatizo yao yakiwa hayajasuluhishwa, kuvunjika moyo, kuchanganyikiwa, na hasira huweza kuleta uchungu ambao husababisha chuki na kulipiza kisasi. Ikiwa watu wawili huingia kwenye ndoa wakiwa na matarajio makubwa kama haya na nia njema, kwa nini sasa ndoa nyingi hushindwa? Kwa namna nyingine, kwa nini wanandoa wengi wanasuluhisha uhusiano ambao haujatimilika?

Kitabu hiki kimetolewa wakfu kwa Mungu na kwa shauku yake kwa kila mwanandoa kupata baraka alizokusudia katika ndoa. Wakati watu wawili wanapoungana kama mume na mke bila mafunzo juu ya kanuni za Mungu na mara nyingi bila mifano ya kimungu kutoka kwenye maisha yao ya zamani, hawa hujikuta hawajui kabisa jinsi ya kutendeana. Huweza kuleta machungu ya zamani, kutengwa na waliowapenda pamoja na mihemko ambayo huongeza changamoto. Kupitia kitabu hiki Mungu atafunua ukweli usiopingika ambao utapaswa kufuatwa, la sivyo matokeo yatakuwa ya kukatisha tamaa na kutokushirikiana; kwa kifupi, maumivu makubwa.

Takwimu zinaonyesha kuwa ndoa nyingi za Wakristo huishia kwenye talaka. Kama watoto wa Mungu na warithi wa ahadi zake zote, kwa nini waamini wanashindwa? Shida ni ukosefu wa maarifa na mafunzo katika kanuni za kibiblia. Kwa kusikitisha, kwa sasa Kanisa haliweki juhudi za kutosha katika eneo hili kugeuza wimbi ambalo linasumbua watu wengi chini ya njia ya uharibifu. Wanandoa wanahitaji sana mafundisho ya kibiblia, kwa kufundishwa na wengine katika ukweli wa Mungu. Waamini wanapojifunza kile ambacho Mungu anataka na kuamua kumfuata kama wanafunzi wa Kristo, watapokea neema na nguvu ya kushinda tatizo lolote.

Mungu anataka kujionyesha mwenye nguvu kwa niaba yetu na anataka tumtukuze katika ndoa zetu; lakini lazima tumkubali pia. Tunajua ndoa ni muhimu kwa Mungu, lakini Wakristo wengi hata baada ya miaka kumi ya ndoa bado wanahisi hawastahili kufundisha mtu mwingine. Fikiria mtu ambaye alikuwa anafanya kazi fulani kwa miaka kumi, si angeweza kujisikia ujasiri *sana* kumfundisha mtu mwingine. Na Mungu anajali zaidi juu ya jinsi tunavyowatendea wenzi wetu kuliko miito yetu.

Unapokamilisha mfululizo huu wa mafunzo kwa maombi, Mungu atafunua kusudi lake kwako kama mume na mke. Maarifa yote yanategemea ukweli wa kibiblia tu. Vitabu hivi vya kujifunzia vitakuongoza kwa kutumia Maandiko na kukupa vielelezo vya vitendo kukusaidia kutekeleza kanuni unazojifunza. Mfululizo pia unakusudiwa kuwa zana ya kuwafundisha wengine. Wakati macho yako yatakapofunguliwa kwa njia ya ajabu ambayo Mungu hutumia kuyabadilisha maisha yako, utaona kwamba wengine wengi wanahitaji msaada wako pia.

> *Bwana Mungu, asante kwa kufunua moyo na mapenzi yako kwetu katika Neno lako. Tafadhali wabariki wale wanaopitia kitabu hiki. Fanya kanuni ziwe wazi. Wape mioyo ya unyenyekevu kuwasamehe wale ambao wamewaumiza na shauku ya kuomba msamaha kutoka kwa wale ambao wamewaumiza. Mungu, utukuzwe ndani ya na kupitia ndoa za wale ambao wako tayari kukufuata. Amina.*

# Utangulizi

Kitabu hiki kimeandaliwa kukuleta kwenye njia ya uanafunzi, ambayo inamaanisha kutembea katika kanuni za Mungu. Tunapotumia maneno kama *kutembea*, tunatumai unaelewa kuwa kuishi chini ya kanuni hizi ni jambo la msingi kama vile kujifunza kutembea.

Malengo ya kitabu chetu ni:

1. Kukuonyesha kuwa Mungu hutoa Kanuni za ndoa,
2. Kukuwezesha kupata mbinu na matumizi ya kanuni hizi, na
3. Kuongoza ndoa na familia yako katika msamaha, uponyaji na umoja unaokuja kwa kumtii Mungu.

Huduma za Uanafunzi katika Familia zipo kusaidia kuelimisha kuhusu mwili wa Kristo katika maeneo muhimu. Kukosa kuwafundisha wengine, kwa leo kunahusiana moja kwa moja na kiwango cha kutofaulu katika ndoa. Na je, tunalijuaje hili? Tunajua kwa njia ya kuona, uzoefu na kupitia katika takwimu zilizothibitishwa kwa wakati huu.

**Mchakato**

Masomo yamegawanywa katika juzuu tano. Anza na juzuu ya 1 na endelea kupitia kila juzuu kwa mpangilio. Kurukia juzuu au sehemu ambayo inachochea shauku yako inashawishi ingawa haishauriwi, kwa sababu kuna mwendelezo katika kila juzuu na kila somo. Kwa mfano, unaweza kutaka kujua mahitaji ya urafiki wa mwanamume au mwanamke, lakini kuna kanuni za kibiblia ambazo lazima ujifunze kabla ya kuzingatia mahitaji ya mwenzi wako kwa njia ya kimungu. Jitahidi kumaliza somo moja kila siku kwa siku tano. Kujijengea tabia ya kusomo kila siku bila kukosa ni ufunguo wa mafanikio ya kiroho.

Kanuni hizi zimejaribiwa na kuthibitika kufanikiwa. Nimeyashuhudia haya katika ndoa yangu mwenyewe na kupitia maisha ya watu, hata katika masomo ya ushauri na ndoa pia. Tafadhali elewa, huu *sio* mwongozo wa "Hatua tano Rahisi za Ndoa." Ufuasi wa kibiblia ni kazi ngumu na inakuhitaji ujikabidhi kwenye mapenzi ya Mungu wakati unapobadilisha mitazamo na tabia zako. Mchakato huu utahitaji kujituma, kujitolea, na kuwa unyenyekevu.

**Kuianza Kila Siku**

- Ona kila somo la kila siku kuwa kama wakati mzuri unaotumia na Mungu wako na mtarajie yeye azungumze nawe kupitia Neno lake.
- Anza kila siku kwa maombi, ukimwomba Mungu akufunulie ni wapi unahitaji kubadilika na kukupa uwezo wa kutumia kile unachojifunza.
- Kuwa na fikra za kutafakari. Usikimbilie kusoma tu ili kusema kwamba umemaliza. Mpe Mungu wakati wa kusema nawe na tafakari juu ya yale unayojifunza.

**Mambo ya Kuzingatia**

- Mafunzo haya ni kipaumbele kipya na utahitaji muda wa kujitolea. Masomo yanapaswa kufanywa kila siku. Ukikosa siku, *usiruke* somo, bali fanya kazi kumaliza masomo yote kwa utaratibu.
- Maandiko yanasema wazi kwamba ndoa ni muhimu kwa Mungu. Ikiwa unajitahidi kumaliza masomo, omba juu ya vipaumbele vyako na ahadi nyingine. Pata msaada wa mshirika anayejituma katika sala ikiwa ni lazima kufanya hivyo.
- Kumbuka, mwenzi wako ni mshirika muhimu katika juhudi hii. Soma pamoja naye au kando yake, lakini kila wakati jadili kile ulichojifunza na jiombee ili uweze kutekeleza mabadiliko yoyote yanayohitajika.
- Masomo yanaweza kutofautiana katika idadi ya mambo yanayowasilishwa. Baada ya kumaliza kila moja, tazama mbele kwa somo linalofuata na kupanga muda wako na Mungu ili kunufaika zaidi.
- Nafasi hutolewa kwa ajili ya kujibu maswali na kurekodi mtazamo yako na sala. Ikiwa umepakua na kuchapisha kitabu hiki cha kujifunzia, tunashauri uweke kwenye mfumo wa kitabu chenye sehemu tatu na ujumuishe karatasi ya ziada kwa ajili ya kuandika mambo binafsi na notisi.

**CHIMBA ZAIDI**

Sehemu hii inaonyesha fursa ya kusoma Maandiko na kuyahusisha na mada inayowasilishwa. Utaijua zaidi Biblia, kanuni za ndoa kibiblia na kile ambacho Mungu anatarajia kutoka kwako kama mwenzi.

**FAILI LENYE UKWELI**
Sanduku kama hili hutoa ufafanuzi wa maneno au vifungu kutoka kwenye Biblia.

Tumechukua tahadhari kubwa kutumia faharasa za Biblia zinazojulikana, zenye sauti za kimantiki na ufafanuzi unaorejelewa inapowezekana. Nyingi ya fasili hizi zinatoka katika kiambatisho R: Faharasa.

**Kujichunguza**
Unapojifunza kanuni za kibiblia, sehemu hii hutoa wakati
wa kujichunguza, kutafuta maeneo ambayo uboreshaji wa kibinafsi unahitajika. Nafasi hutolewa kwa ajili ya kuorodhesha ufahamu, maungamo na maombi ya nguvu na hekima ya kufanya mabadiliko hayo. Kipengele kimojawapo katika mchakato wa Uanafunzi ni uwajibikaji binafsi. Ikiwa Mungu amekufunuliwa kuwa umemkosea mwenza au mtoto wako, basi tubu dhambi yako kwao na uombe msamaha. Jizoeze kufanya hivyo hata kama utafanya pasipo kujulika kwa yeyote.

***MPANGO KAZI***

Baada ya kusoma kanuni za kibiblia, sehemu hii inakupa changamoto ya kuchukua hatua na kutumia kile ulichojifunza katika ndoa yako. Ili kuwa wanafunzi wa kweli lazima tuelewe kwamba Mungu hatamani tu tuweze kukua katika maarifa, lakini pia anahitaji tuyaishi.

**Rasilimali Viambatisho**

Tafadhali pata faida kupitia viambatisho mwishoni mwa kitabu hiki cha kujifunzia. Vipo kwa ajili ya ukuaji wako na tunavirejelea katika kitabu hiki cha kujifunzia. Kabla ya kuanza safari hii nzuri, tafadhali jaza *Kiambatisho A: Barua ya Kujitolea*.

**Mwongozo kwa Kiongozi**

Mwongozo kwa msomaji unapatikana kwenye *FDM.world under free Ministry downloads*. Vifaa vyote kwenye Tovuti yetu hujikita katika uanafunzi na hutolewa bure.

## Somo 1

## Safari Binafsi

Mafunzo haya yote yamejikita katika mpango wa Mungu kwa ajili ya ndoa, ambayo inaleta maana kwa sababu yeye ndiye aliyeumba mwanamume na mwanamke ili waungana katika umoja huu mtakatifu. Kuona ndoa kama huduma kunawasilisha imani yetu kwamba msingi wa ndoa yenye mafanikio unahitaji mawazo ya huduma. Wote wawili mume na mke sasa wako katika huduma ya wakati wote, wakihudumiana kwa madhumuni yaliyokusudiwa na Mungu. Mungu hakutuweka hapa duniani akitarajia kwamba tungepanga ndoa sisi wenyewe. Katika Biblia Neno la Mungu lina taarifa kamili katika kutuongoza kwenye maeneo yote ya mahusiano.

Katika Neno lake, Mungu hatuonyeshi tu makusudi yake juu ya ndoa bali pia jinsi ya kuanzisha msingi wa ndoa yenye mafanikio. Kupitia mafunzo haya, utajifunza asili ya upendo wa kweli, ambao ni hitaji kuu la urafiki wa wanadamu. Zaidi ya hapo, utayachukulia mahitaji mengine ya ushirika kuwa ya kipekee kwa mume au mke kwa sababu, kama unavyojua, wanaume na wanawake ni tofauti. Si ndivyo tulivyo? Hadi sasa, uzoefu unapaswa kuwa umetufundisha kuwa sisi ni tofauti kimwili na kihisia.

Msingi hapa ni kukielewa kile ambacho Neno la Mungu linasema juu ya mahitaji ya urafiki. Bila hiki, tunakuwa tu na maoni yetu binafsi juu ya kile tunachohitaji au tunachotarajia kutoka kwa mtu mwingine. Mtazamo wa "Nadhani __________ ndio ninachohitaji" hutoa matarajio mengi yasiyo ya kibiblia ya kile sisi tunachoamini kwamba mke au mume anatakiwa kutoa katika uhusiano wa ndoa na kisha tunajikuta taabuni. Mahitaji yetu ya urafiki tuliopewa na Mungu yanapotambuliwa na kutimizwa kulingana na mpango wake tutapata utimilifu katika ndoa.

Kabla mafunzo haya hayajakamilika, utajifunza taarifa muhimu juu ya uongozi wa kikuhani ambao ni wito wa mume uliotolewa na Mungu, lakini pia ni taarifa zenye thamani sawa kwa wake. Wanawake tiweni moyo kwa umuhimu mkubwa wa jukumu lako la kibiblia, ambalo ni kumsaidia mume wako katika huduma ambayo Mungu amemtia mafuta kuitimiza nyumbani. Kwa kufanya hivyo, utamsaidia mumeo kufanikiwa na umsaidie kuamini kwamba anaweza, kwa neema ya Mungu, awe kiongozi anayemcha Mungu na kumtumaini ili aweze kupata kila anachohitaji kwa ajili ya mafanikio.

Mungu anataka kujionyesha kuwa mwaminifu. Anapenda kujionyesha. Yeye anatenda kweli. Anataka watu waone wema wake, wamtukuze kupitia ndoa ili wengine ambao wanasumbuka watulie na kujiuliza, *Je! Wana nini ambacho hatuna?* Mungu anatuita tuwe nuru katika ulimwengu huu wa giza.

Kitabu hiki cha mafundisho ya ndoa kina suluhisho la matatizo yako, majibu ya maswali ambayo umekuwa ukijiuliza. Ikiwa umezaliwa katika familia ya Mungu kupitia wokovu katika Yesu Kristo, anakuita mtoto wake na ameweka Roho wake Mtakatifu ndani yako kukufundisha kuhusiana na Neno lake basi, una kila unachohitaji kwa mafanikio. Sehemu yako ni kutamani kutimiza mapenzi yake katika ndoa yako na hiyo ndiyo njia ya kuvuna baraka za Mungu. Usife moyo, endelea mbele.

> Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho. (Wagalatia 6: 7-9)

Baada ya miaka mingi ya kutoa ushauri na saha nimegundua kuwa Wakristo wengi hawajui mapenzi ya Mungu ni yapi katika ndoa zao.

**Mtegemee Mungu**

Mungu anataka kukujulisha kwamba anaweza kukupa chochote unachohitaji. Unaposoma mistari hii, dai ahadi zake kwa imani.

> Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. (2 Petro 1: 3-4)

Petro anasema Mungu ametupa "vitu vyote vinavyohusu maisha," ambayo ni pamoja na zana zote muhimu za kujenga ndoa ya kibiblia. Mafundisho yetu ni Neno la Mungu na kama inavyoahidi katika aya ya 3, ni kwa "uweza wake wa kimungu" ndio tutafanikiwa.

**FAILI LENYE UKWELI**

*Nguvu - Dunamis* (Kigiriki). Nguvu ya au uwezo wa kufanya kile ambacho ni Mungu tu anayeweza kufanya. Chanzo chetu ni "Nguvu zake za kimungu."

*Maarifa - Epignosis* (Kigiriki). Kushiriki kikamilifu katika kupata maarifa. Tunashiriki asili ya kimungu na tunaahidi "kupitia kumjua yeye."

Tunapozaliwa mara ya pili kwa njia ya imani katika Yesu Kristo, tunapokea Roho Mtakatifu (Waefeso 1: 13–14) na nguvu iliyomfufua Yesu kutoka kwa wafu huanza kufanya kazi ndani yetu (Waefeso 1:19-20). Lakini usikose kujua ya kuwa haya yote yanaweza kupatikana tu "kupitia kumjua yeye."

Nguvu ya Kristo huathiri mwamini na huja tu kupitia wokovu na kukaa ndani yake na Neno lake. *Kukaa* kunamaanisha "kukaa ndani" na ina maana zaidi ya ujuzi wa kichwani, ufahamu wa kiakili juu ya Yesu. Inamaanisha kupokea Neno kama ukweli na kisha kuwa mtiifu.

Tunapokaa ndani ya Kristo, sio tu tunapata maarifa ambayo yanaweza kutubadilisha, tunastahili pia "ahadi kubwa na za thamani" kutoka kwa Mungu ambaye ni mwaminifu kwa asilimia 100. Na, kama "mshiriki wa uumbaji wa asili wa kimungu," unaweza kupata hekima isiyo ya kawaida na nguvu kwenye ndoa yako, kulingana na ahadi zake.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua Nini ambacho Mungu amehadi katika Mistari hii.

> Kwa kuwa Bwana Mungu ni jua na ngao,
> Bwana atatoa neema na utukufu,
> Hatawanyima kitu chema,
> Hao waendao kwa ukamilifu. (Zaburi 84:11)

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Bali utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa. (Mathayo 6:33)

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

**Kujichunguza**

Je! Ukweli huu unaathirije mtazamo wako katika ndoa yako?

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua kanuni zilizomo katika Maandiko haya pamoja na kile ulichoahidiwa.

> Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho. (Wagalatia 6: 7-9)

> Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. (2 Petro 1: 3-4)

**Kuhoji Uzoefu wa Zamani**

Wengi wetu tunadhani kuwa wazazi wetu walitumia falsafa ya "Kupiga na Kukosa" katika kutatua shida kwenye ndoa zao.

Ukiangalia nyuma kwenye maisha ya wazazi wako, unaamini kwamba walikuwa na mpango mzuri wa kibiblia katika kutendeana? ___ Ndio/Hapana

Je! Njia zinazotumika katika ndoa yako mwenyewe (mitazamo, matarajio, na mawasiliano) zote zinategemea kanuni za kibiblia? ___ Ndio/Hapana

Kwa kawaida watu huiga matendo mazuri ambayo wazazi wao walifanya, hutupilia mabli mbaya na hufanya mengine yanayostahili. Hiyo inamaanisha kwamba chaguzi zetu nyingi hutokana na mtu binafsi na uzoefu alionao. Kwa kuwa mume na mke hawakuwa mambo yanayofanana, kila mmoja huleta uzoefu wake wa mwanzo kwenye maisha ya sasa na kisha hupotea katika harakati za kujaribu kupata njia inayokubalika kwenye ndoa. Katika mazingira kama haya, ukomavu wa kifikra hauwezi kuonekana kwa sababu ya mitazamo yao binafsi, pamoja na tabia nyingi za uharibifu zilizojitokeza njiani.

Kwa kuyatambua haya yote, tunapaswa kuwa na shauku ya kujifunza kanuni muhimu ya kwanza ya ndoa, ambapo ni muhimu kutegemea Neno la Mungu. Mawazo kwamba, "Nilidhani ikiwa ningefanya kazi vizuri kuliko wazazi wangu, basi ndoa yangu ingekuwa bora kuliko yao!" sio jambo jipya, lakini sio msingi wa mafanikio pia. Biblia lazima iwe msingi wa ndoa yako na mchakato wa kufanikiwa ni matumizi ya hekima ya Mungu. Mungu anataka kila mwenzi ajue kuwa yeye ametoa habari zote muhimu na neema kwa *kila mmoja* ambaye anatamani kwa dhati kuyashika mapenzi yake.

## CHIMBA ZAIDI

Tambua kile Mungu anasema juu ya kumfuata yeye au kufuata hekima yako mwenyewe.

> Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote,
> Wala usitegemee akili zako mwenyewe,
> Katika njia zako zote mkiri yeye,
> Naye atayanyoosha mapito yako. (Mithali 3: 5-6)

Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, Lakini mwisho wake ni njia za mauti.(Mithali14:12)

Katika Maandiko haya, Paulo alituamuru *tutembee* katika njia fulani, ambayo ni njia maalumu:

> Basi kama livyompokea Kristo Yesu Bwana, endeni vivyo hivyo katika yeye, wenye shina na wenye kujengwa katika yeye mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa, mkizidi kutoa shukrani. (Wakolosai 2: 6-7)

Je! Tunapaswa kutembea vipi? Ikiwa unatembea kwa njia hiyo, itaathiri vipi ndoa yako?

Paulo alifanya ulinganisho unaofaa katika aya ya 8. Alisema *tahadhari*, ambayo inamaanisha "jihadharini na endeleeni kujihadhari."

> Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo. (Wakolosai 2: 8)

Hatari ni ipi? Ni nini chanzo cha hatari hii? Kulingana na Maandiko haya, tunahitaji kujihadhari na nini?

Tunapaswa kupata wapi taarifa zetu, hekima, na maagizo?

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua matokeo yanayowezekana hapa chini, mazuri na mabaya.

> Mtu asikudanganye kwa maneno yasiyo na maana, kwa kuwa, kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu huwajia wana wa uasi. (Waefeso 5: 6)

> Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kibisa, mkizaa matunda kwa kila kazi njema na kuzidi katika maarifa ya Mungu. (Wakolosai 1:10)

> Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyani yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye. (Wakolosai 3:17)

***MPANGO KAZI***

Mbali na Neno la Mungu, nguvu na hekima, hatuwezi kuwa wenzi ambao Mungu anatutaka tuwe. Ikiwa una shaka yoyote juu ya kuwa mtoto wa Mungu, fungua *Kiambatisho B: Kujitolea Maisha yako kwa Kristo* na ufuate miongozo kutoka kwenye Neno lake juu ya jinsi unavyoweza kuja katika familia yake.

## Somo la 2

## Hapo Mwanzo

Hapo mwanzo, Mungu aliumba mwanamume na mwanamke na kisha akabuni umoja kamili kwa wawili hao umoja ambao tunaujua kama ndoa.

> Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. (Mwanzo 2:24)

Ufafanuzi wa ulimwengu kuhusu maana ya ndoa umebadilika sana, lakini muundo wa asili wa Mungu haujabadilika. Uaminifu kutoka kwenye mtazamo wa kibiblia utatufanya tukubali kwamba mabadiliko mengi hayakuwa ya kimungu na kwa sababu hiyo ndoa na familia vimepata tabu sana. Sababu ya msingi katika hili ni kutokujua kwetu Neno la Mungu, haswa muundo wake na kusudi la ndoa. Ingawa maarifa haya yamekuwa yakipatikana, watu hawaelekezwi au kufundishwa juu ya kanuni za ndoa.

Ukosefu wa mafundisho ya kibiblia, au kukataa kabisa mamlaka ya Mungu, huwaacha wanandoa kufuata mwelekeo wa ulimwengu au njia zao wenyewe. Kwa muda sasa, kumekuwa na ongezeko la takriban asilimia 400 ya wanandoa wanaoishi pamoja bila kujitoa kikamilifu katika ndoa. Sasa inakubalika kabisa kwa mwanamke kupandikizwa mimba au kuasili mtoto bila uwepo wa mume au mwenzi wa kiume. Vyama vya jinsia moja vimeongezeka na vinachukuliwa kama mazingira yanayokubalika ya kulelea watoto. Mifano mingi ipo katika vyombo vya habari maarufu, mtandaoni na katika machapisho ambamo huinua maoni potofu ya Hollywood na wanaongoza katika maeneo haya ya uharibifu.

### Usikate Tamaa

Rafiki, usiruhusu mienendo ya kitamaduni ikukatishe tamaa juu ya ndoa. Shetani angependa kuchora picha mbaya, lakini jua kwamba Mungu ni mkuu na ana nguvu zaidi. Utafiti unaonyesha kuwa kati ya watu wanaochagua kuoana, muungano huo bado una nguvu na unaleta furaha kubwa na utimilifu. *Habari Njema Kuhusu Ndoa* na Shaunti Feldhahn ulipingana na takwimu kwamba asilimia 50 ya ndoa huishia kwenye talaka, katika maisha ya kidunia na ndani ya Kanisa. Utafiti wa Feldhahn ulifunua kwamba asilimia 72 ya watu walioolewa bado wako na wenzi wao wa kwanza na kwamba asilimia 80 ya ndoa zote zina furaha. Miongoni mwa Wakristo wanaoshika imani yao, waligundua kwamba kuhudhuria kanisani kila wiki peke yake kunashusha kiwango cha talaka kwa kiasi kikubwa kwa asilimia 25 hadi 50 ya kiwango cha talaka kwa mwaka. "Kwa hakika, ikiwa wenzi wote wawili walisema 'Mungu ndiye muhimili wetu,' asilimia 53 ya wenzi hao walikuwa katika kiwango cha juu kabisa cha furaha ya ndoa" (Feldhahn, ukurasa wa 78). Takwimu hizi zinapaswa kutupa matumaini makubwa na kutuhamasisha kutafuta mapenzi ya Mungu katika ndoa zetu.

Mwaka 2014, utafiti wa kitakwimu kutoka kwenye Kikundi cha Barna ulionyesha kwamba karibu asilimia 40 ya familia nchini Marekani ziligawanywa kama familia ya mzazi mmoja. [1] Hata hivyo, takwimu hizi zinajumuisha watu ambao ni wajane, talaka, au wanaoanzisha familia bila mwenzi. Karibu asilimia 39 ya familia hizo ni za mchanganyiko (watu walio na watoto ambao wanaoa tena baada ya talaka au kifo) na chini ya asilimia 3 wanalelewa na babu na bibi. Hii inabakiza asilimia chini ya 20 tu katika kundi linalojulikana kama familia ya jadi, ambayo inamaanisha mume na mke wa asili. Bila kuwa mkali au kuhukumu kwa njia yoyote, naamini familia ya jadi ndio imeumbwa kikamilifu kulingana na muundo wa Mungu na mapenzi.

Ingawa "Tamaduni" haijumuishi talaka, najua pia Mungu anaelewa na kuzingatia familia zote zilizochanganywa na za mzazi mmoja kama sehemu ya mapenzi yake na kuruhusu. Mungu yuko nyuma kwa asilimia 100 kwa mtu yeyote anayetaka msaada wake na katika hali hizi, yeye bado "hufanya mambo yote kulingana na shauri la mapenzi yake", rejelea, Waefeso 1:11.

## Mabadiliko katika Maana

Leo, tunaona mpango wa Mungu kuhusu ndoa na familia sio tu kwamba unabadilika lakini kwa hakika unashambuliwa. Mwaka 1944, *Kamusi ya Webster* ilifafanua *ndoa* kama "hali ya kuolewa, kuunganishwa na mtu wa jinsia tofauti kama mume au mke; uhusiano wa pande zote wa mume na mke kwa kusudi la kuanzisha na kudumisha familia." Mwaka wa 2018, ufafanuzi huo umebadilika na kuwa "hali ya kuwa wamoja kama wenzi wa ndoa katika uhusiano wa makubaliano na wa kimkataba unaotambuliwa na sheria; kitendo cha kuoa au ibada ambayo hali ya ndoa imetekelezwa; muungano wa kamapenzi au wa karibu zaidi" ( *Merriam-Webster's Collegiate Dictionary* ). Ni nini kilicholeta mabadiliko, na inamaanisha nini?

Ufafanuzi unaobadilika unaonyesha mmomonyoko wa taratibu wa msingi wa kiroho wa ndoa katika jamii yetu. Maneno muhimu katika ufafanuzi wa kwanza, "kuungana… kama mume au mke," inaonyesha kuungana na kuwa wamoja na mtu wa jinsia tofauti. Kifungu hiki kinatoka kwenye Bibilia (Mwanzo 2:24). Kadiri mafunzo haya yanavyoendelea, yatafunua maelezo kutoka kwa Mungu ambayo hufafanua muundo wake wa asili wa ndoa, sio mazoea yanayotokana na maoni ya kibinadamu au tamaduni wa kiulimwengu.

Ufafanuzi wa maana ya ndoa kwa mwaka 1994 kutoka kwenye Webster unarejelea katika "uhusiano wa pande zote," hali ambayo inamaanisha kupewa au kuhusiana kwa kila mmoja kwa viwango sawa ili kukidhi mahitaji ya urafiki wa kila mmoja. "Kuanzisha na kudumisha familia" inamaanisha kuanzisha msingi imara wa kukuza maisha na mwenendo fulani na kulea watoto. Mabadiliko ya maelezo yanaonyesha jinsi dhana msingi zilivyobadilishwa na jinsi ndoa na familia zinavyo haribika. Mpango wa Mungu juu ya ndoa hauwezi kutambulika katika kaya nyingi.

Waamini wote wanahitaji kujua mioyoni mwao kwamba, Mungu ndiye muumbaji wa ndoa na kwamba mapenzi na kusudi lake la ndoa halijabadilika kamwe. Ingekuwa vema kwa Mungu kubuni kitu muhimu na cha muungano mzuri kama ndoa na kisha aseme, "Wewe tatua hili kila kitu mwenyewe."

Ndoa ni ngumu. Nipo ndani ya ndoa tangu 1980, najua inahitaji kufanyiwa kazi. Msifu Bwana wakati unapogundua ukweli wake na kutumia kanuni za kibiblia kwa kuishi ndani ya Kristo na kuifanya ndoa kuwa nzuri zaidi. Hivyo ndivyo Mungu atakavyo, anataka iwe nzuri kila mwaka. Kila mwaka unaopita, nampenda sana mke wangu na ninaweza kukwambia yuko pamoja nami pia.

Tunapoweka muda wa kujifunza ukweli na makusudi ya Mungu katika ndoa, kudumisha na kutekeleza kanuni hizi, ndoa inakuwa tajiri zaidi. Mungu anataka kutukuzwa katika ndoa zetu, anatamani kudhibitisha upendo wake kwetu kwa kuonyesha kwamba yuko *pamoja* nasi na *kwa ajili* yetu.

### Matarajio Sahihi katika Ndoa

Kila mtu huingia ndani ya ndoa na matarajio. Ni *Kila mtu*, huenda yasiandikwe, lakini yapo: matarajio juu ya kile unachostahili na nini unapaswa au utarajia kukitoa.

**FAILI LA UKWELI**
*Marajio*- Matamanio au dhana ya kitu kinachotokea, ni kiwango kinachotarajiwa.

Labda umesikia usemi usemao, "Upendo ni upofu." Ni kweli, kuanzia uchumba hadi kuingia kwenye ndoa, kila mtu anaonyesha upande wake mzuri kwani mapenzi ya kimahaba huwabeba pamoja na matarajio yenu kuwa yote yatabaki kama yalivyo. Hata hivyo, fungate linapoisha, mnaanza kuishi pamoja, kila mmoja na dhambi zake, ukweli wa kila jambo unajidhihirisha na kile mnachokipitia *sio* kile kilichotarajiwa na kila mmoja wenu.

**Kujichunguza**

Ulitarajia nini kutoka kwenye ndoa yako au kutoka kwa mwenzi wako? Kila mmoja aandike tofauti na mwenzake, kisha mjadili kwa pamoja.

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

**Matarajio ya kijinga**

Niliingia ndani ya ndoa nikileta mitazamo na matarajio ambayo hayakuwa hata karibu na ukweli wa Mungu. Nilidhani alikuwa na bahati kuwa na mimi. Nilifikiria sana juu ya hilo! Nilidhani nilikuwa nimemkamata, mpumbavu kabisa, *Alikuwa* Amekamatika. Nilitarajia kuwa siku za mwisho wa juma ningeweza kufanya kila kitu ninachotaka, kwa wakati huo, nilikua na pendelea kukimbia, kupiga mbizi, kuvua samaki na uwindaji; hivyo nilikua na shughuli nyingi.

Nilimwambia, "Ikiwa sitakuwa kitu chochote nilichopanga kufanya, basi tutafanya kitu chochote pamoja." Na bado aliamua kuoana na mimi. Nilidhani tu hivi ndivyo maisha yalivyokuwa.

Matarajio mengine yalikuwa kutumia pesa *zangu* jinsi nilivyotaka bila kumuhusisha au kupata maoni kutoka kwake. Pia nilitaka abaki mrembo na kukidhi mahitaji yangu yote ya kimwili, kuwalea watoto wetu na kuweka nyumba yetu safi. Hiyo sio ngumu sana, sivyo? Je! Hiyo ni haki kweli? Ninyi wanawake mnaweza kufikiria huyo anaonekana kama mume wako. (Kuna matumaini kwake pia)

Sikujua mengi zaidi. Kwa hivyo tunajifunzaje kuwa waume na wake wazuri? Tunakumbuka vile wazazi wetu walivyofanya na ambavyo hawakufanya na kufuata mwongozo wao na tunabadilika kuanzia hapo. Mambo kama haya yanaweza kukutatiza zaidi ikiwa unatoka katika familia yenye mzazi anaejitegemea au familia iliyochanganywa au kukulia kwa babu na bibi au katika nyumba za kulea watoto. Halafu kuna nyumba ambazo mzazi, au wazazi wote wawili, hawapo kwa sababu za kikazi.

Sisi sote huoana tukiwa na matarajio mabaya na kusababisha kutamauka, kukata tamaa, na kutoridhika. Katika miaka yetu miwili ya kwanza ya ndoa, mke wangu alitumia wakati

wake mwingi akijaribu kunibadilisha. Baadhi yenu mnaweza kuhusisha. Aliendelea kujaribu kuonyesha udhaifu wangu, jambo ambalo lilinikasirisha sana. Sasa ndo ninagundua kuwa matarajio yangu yalikuwa yakibinafsi kupita kiasi na mbali kabisa na mapenzi ya Mungu, lakini sikua nikijua hilo wakati huo. Niliweka wazi maono yangu kabla ya ndoa yetu, kwa hivyo kwanini aendelee kujaribu kunibadilisha? Mke wangu alikuwa akifanya tu mambo yote ambayo wanawake hufanya kwa kawaida yao, yaani kumboresha mwanaume.

**Kuguswa na Kubadilika**

Wakati tuliposhiriki katika mafungo ya kwanza ya urejesho kwa ndoa yetu, mimi na mke wangu tukawa Wakristo na tulikuwa tukihudhuria kanisani. Nilidhani, *Loo, sasa wote wawili tutaenda vizuri! Hatimaye, mwanamke yule atakisikia kile ambacho amekuwa akikosea kwangu; kwa sababu angalau ninajua Biblia haimfundishi mke kuendelea kujaribu kumbadilisha mumewe.* Nilikwenda na wazo kwamba mke wangu ataenda kusikia kile ambacho alikuwa akikikosea na nikawa najaribu kukisia mawazo yake pia, kwamba naye aliwaza nilivyowaza mimi. Sisi sote tulifikiri tutasikia kitu ambacho kitambadilisha mwingine kuwa bora.

Tulipoenda kwenye mafungo, asifiwe Bwana kwamba mzungumzaji alifundisha kutoka kwenye Bibilia na sisi sote tukamaliza wikiendi hiyo tukishangaa kabisa ni kiasi gani Mungu anasema juu ya maana ya kuwa mume na mke. Tukifikiria, jinsi tulivyotendeana na jinsi tulivyofanya kila kitu kinyume kabisa na kile ambacho Neno la Mungu lisemavyo; hakika sisi sote tulimaliza wikendi tukiwa tumeguswa sana na Mungu. Nilimwita mzungumzaji baada ya mafungo nikamwambia, "Ndugu umetuguswa sana mimi na mke wangu! Nahitaji msaada." Mtu huyu alinifundisha kwa miaka iliyofuata. Huwezi tu kwenda kwenye mafungo ya wikendi moja na kusema, "Sawa, nimeelewa." Hayo ni mawazo ya kutamani tu kubadilika na ni ujinga.

Mimi na mke wangu tunaweza kusema, "Kweli, tulienda kwenye mkutano wa ndoa." Lakini ni kiasi gani tuliguswa na mafunzo na kisha kuanza kuyafanyaia kazi katika maisha yetu? Pindi sisi sote tulipoingia katika huduma hii na kuanza kujifunza Biblia, Mungu alifanya mabadiliko ya kimiujiza katika ndoa yetu ambayo hatukuweza kujizuia isipokuwa kuwashirikisha wengine.

**Huduma ya Ndoa**

Wakati huo katika safari yangu ya Kikristo sikujua juu ya dhana ya utumishi, mchakato maalum wa kujifunza na sehemu muhimu inayohusika katika kutumia ukweli wa kiroho.

Nilianza kushirikishana na watu mambo ambayo nilikuwa nikijifunza na baadye mchungaji wangu alinipigia simu na kusema, "wewe, unawaambia nini watu? Unawabariki na wanasema kweli unawahudumia. " Nakumbuka nilifikiria, *Mh, Mungu anaweza kutumia mjinga kama mimi.* Kisha mchungaji wangu akaniuliza, "Je! Unaweza kuomba kuhusu kuanzisha huduma ya ndoa?"

Kwa hivyo mimi na mke wangu tulianza mafunzo kidogo ya Biblia juu ya ndoa ambayo yalitoka kwa wenzi watatu hadi zaidi ya thelathini kwa kipindi cha miezi mitatu. Mungu alianza kufanya muujiza kama huo katika maisha yetu na ya wengine. Niliona,*ama kweli Mungu, hii ni ya kushangaza.* Ndipo nikaanza kuongeza juhudi zaidi na kusoma mambo yote ninayoweza kujua juu ya ndoa katika Biblia. Tulishuhudia tena na tena kwamba ikiwa watu wamejitolea kweli kufanya mapenzi ya Mungu na kufuata kile Neno lake linasema kuhusu mume na mke, basi watapata uponyaji na baraka. Na nilijua ninaweza kufanya huduma hii kwa maisha yangu yote. Lakini baada ya miaka mitatu, Mungu aliniongoza kuwa mchungaji mchanga wa vijana. Nilidhani kuna mtu alifanya makosa. Lakini kumbuka, Mungu ana mpango kila wakati.

Nilikaa miaka minne na nusu nikiwa mchungaji wa vijana wa kawaida tu. Katika mafunzo mazuri ya Mungu, alifanya mengi katika maisha yangu ili kuniweka katika mazingira haya ya kuniwezesha kujifunza na kuwafundisha watu sio tu juu ya ndoa lakini pia juu ya malezi. Kufanya kazi na vijana kulinipa ufahamu na mitazamo ya kipekee juu ya familia. Mungu alikuwa akiniandaa kugusa mamia ya maelfu ya watu. Huo ulikuwa mpango wake, lakini ilibidi nikubali kile alichonifundisha na kutumia kanuni zake kabla sijaona mkono wa Mungu ukifanya kazi na kupata maarifa ya kweli ya kibiblia.

Sijiinui juu mwenyewe au kujisifu juu ya kitu chochote, kwa maana sina chochote kinachoweza kutoka kwangu. Ninajua tu kwamba wakati nipolimwamini Mungu na kutumia kanuni zake, niliona kile alichofanya katika maisha yangu na familia. Na hivyo ndivyo Mungu anavyotaka, yeye anapenda kujionyesha kupitia sisi.

**Matarajio mabaya**

Ukiingia ndani ya ndoa na matarajio mabaya na hujui jinsi ya kudumisha ndoa yako

kulingana na Neno la Mungu, swali sio je, utapata shida? swali la kuuliza ni *shida ngapi?*

Ikiwa utatumia $ 30,000 kununua gari, unatarajia gari hilo litaonekana na kukimbia vizuri kama siku uliyolinunua kwa angalau miaka ishirini. Unaamini kuwa kwa sababu ulitumia pesa nyingi, ungeendesha miaka yote ishirini kwa kutumia tanki moja la mafuta, mafuta yasingehitaji kubadilishwa, breki na matairi yangedumu na ingebaki kung'aa bila kusafisha au kutia nta.

Ikiwa hayo yalikuwa matarajio yako, ni nini kitatokea kwa mara ya kwanza unapoingia barabara kuu na kuishiwa mafuta? Unaweza kutoka nje ya gari, ukiwa umekasirika na

ukajiuliza kuna shida gani kwenye tanki. Unaweza kumwambia muuzaji wa mafuta barabara kuu kwamba gari iliacha tu kukimbia ghafra. Na angekutazama na kujiuliza, mtu mzima kama wewe ulikuwa unatumia dawa za kulevya au uu mjinga na unajielezea kuwa umeishiwa na mafuta.

“Unamaanisha nini, *nimeishiwa mafuta*? Kwani natakiwa niweke mafuta kwenye gari? ”

Baada ya kuvutwa hadi kwenye kituo cha kujaza mafuta, utagundua itakuchukua tu kilometa 250 na uhitaji kujaza tena, utakasirika.  Hatimaye utafikia hatua ya kukubali wazo hilo, unaweza kupata pigo. Afisa mwingine anaweza kukwambia kuwa matairi yako ni kipara. Ukifika dukani, unaweza kukuta kwamba unahitaji matairi mapya *na* breki. $ 1,200 nyingine na kwamba unatakiwa kutoa pesa. Miezi sita baadaye, gari linaweza kuanza kutoa moshi na utarudi dukani tena ila mara hii si kwa ajili ya kuweka mafuta tena.

Ikiwa una matarajio mabaya, utafadhaika na kuanza kuamini kuwa umedanganywa au kudhulumiwa. Hivyo ndivyo utakavyo amini. Na ukweli ni kwamba haukudanganywa hata kidogo, bali ulikuwa na matarajio mabaya ya kile ambacho gari hilo lilitakiwa kukifanya, jukumu lako wewe lilikuwa ni kuendelea kulitunza.

Siku hizi watu wengi wanafikiri walidanganywa katika ndoa. Wakati waume na wake wanapoingia kushauriwa, naweza kona hilo hata kwa jinsi wanavyokaa. Wote wawili wana kaa kila mtu na pembe yake ya kochi, wakinitazama kama wanawaza, "sio siri, nimefanya maamuzi mabaya kuja hapa!" taswira hio inakuwa imejaa kwenye nyuso zao na lugha zao za mwili. Baada ya kujifunza kutoka kwao kile walichotarajia kutoa na kupokea kutoka kwa kila mmoja, naweza sasa kuelewa ni kwa nini hawana furaha na wanajihisi hawajatimilika. Ni kweli kabisa huwa tunafanya makossa ya kipumbavu, lakini makosa mengi yanatokana na sisi kuwa na matajio mabaya na ndoa hizo.

Mungu ametupa mwongozo wa matengenezo yaani, Neno lake. Biblia ina kila kitu tunachohitaji kujenga na kudumisha uhusiano unaojitosheleza. Kwenye ndoa huwezi ukafika mahali ambapo utasema, “Loo, nimemaliza. Sina ulazima wa kuwekeza kwa mke wangu au mume wangu tena.” Ni uwekezaji endelevu kwa kila mmoja kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua kile ambacho mistari hii inasema juu ya kuwekeza wakati wa kujifunza mapenzi na matarajio ya Mungu.

> Jitahidi kujionyesha kuwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari ukitumia kwa halali neno la kweli. (2 Timotheo 2:15)

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

> Kila njia ya mtu ni sawa machoni pake mwenyewe,
> Bali Bwana huipima mioyo. (Mithali 21: 2)

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

> Maagizo ya BWANA ni ya adili, huufurahisha moyo.
> Amri ya Bwana ni safi, huyatia macho nuru. (Zaburi 19: 8)

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

Unapoenda kwenye Neno la Mungu, kujifunza juu ya makusudi yake katika ndoa na mahitaji yako ya ushirika kama mume na mke na kujitolea kufuata maagizo yake, utavuna utimilifu wa ndoa ambao Mungu amekupangia. Unapojikuta katika hali mbaya, haupati furaha na amani, kumbuka Kristo anasema nini.

Yesu hakusema nenda kwenye saikolojia ya ulimwengu au falsafa, wazazi wako na mifano yao au marafiki, bali njoo kwa Bwana na kwa njia ya Neno lake, hapo utajifunza hekima ya kibiblia, ambayo itakupa matarajio ya kimungu.

Yesu ni mfano bora wa kuwa na akili inayozingatia kutimiza mapenzi ya Baba. Unaposoma Injili, utagundua kwamba viongozi wa dini walijaribu kumuondoa kwenye njia, lakini Yesu alijua jambo la maana ni kutimiza yale Mungu anayoyasema.

> Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka. (Yohana 6:38)

> Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe, kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyon a hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu sitafuti mapenzi yangu mimi bali mapenzi yake aliyenipeleka (Yohana 5:30)

Yesu akawaambia, chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikamalize kazi yake. (Yohana 4:34)

Yesu alikuja kutimiza mapenzi ya Baba yake, kutekeleza mpango na kusudi lake. Angalia kwamba *chakula* chake kilikuwa kutimiza mapenzi ya Baba. Tunahitaji kuyaona maisha kwa njia hiyo, ambayo ni pamoja na kulinda ndoa zetu.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua nini ambacho mistari hii inasema juu ya mapenzi ya Mungu na kile tunachopaswa kufanya.

> Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema ya kumpendeza na ukamilifu. (Warumi 12: 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

> Wala si kwa utumwa wa macho tu kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kama watumwa wa Kristo, mkitenda yampendezayo Mungu kwa moyo. (Waefeso 6: 6)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Kama Warumi 12: 2 inavyosema, sisi sote lazima tuthibitishe mapenzi ya Mungu ni nini na njia pekee ya kufanya hivyo ni kujua Neno lake.

## Somo la 3

## Mungu, Muumbaji wa Ndoa

Ndoa halali nchini Marekani kitamaduni imekua ni kati ya mume mmoja na mke mmoja. Hii ni kwa sababu ya mitazamo ya Kikristo ya wale ambao walianzisha nchi hiyo, ingawa kwa sasa, ufafanuzi huo wa ndoa unashambuliwa. Katika tamaduni nyingine, hekima ya mwanadamu imeshinda na kusababisha mitala. Wanawake wanachukuliwa kuwa mali ya kumilikiwa na wana haki chache kama wake na hata kama mama wa watoto wao. Falsafa ya leo kwa ulimwengu wote ni "Tutakaa pamoja kwa muda mrefu kama utanifurahisha." Kulingana na utafiti wa Pew wa mwaka 2010, "Karibu Wamarekani wanne kati ya kumi wanasema ndoa imekuwa mambo ya kizamani." [2]

Hata hivyo, kinyume na kanuni hizi za kitamaduni, Mungu wa kweli, muumbaji wa ndoa, ana mengi ya kusema juu ya tabia njema, mitazamo na matarajio ya waume na wake. Mungu pekee ndiye anayeshikilia ukweli wa jinsi anavyotaka ndoa ifanye kazi, maana yeye ndiye muumbaji. Maandiko yafuatayo yanafafanua mtazamo wa Mungu na tofauti kati ya njia za Mungu na za mwanadamu.

> "Maana mawazo yangu si mawazo yenu,
> Wala njia zenu si njia zangu," asema Bwana. "
> Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu kuliko nchi,
> Kadharika na njia zangu zilivyo juu kuliko njia zenu.
> Na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. " (Isaya 55: 8–9)

***MPANGO KAZI***

Andika sala kwa Mungu. Ikiwa umekuwa ukifuata njia zako mwenyewe, ukiri kwake na umwombe msamaha.
Jitolee kujifunza mapenzi yake na kufuata njia yake katika ndoa yako.

____________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

Mungu hakuachi ukibashiri juu ya mpango wake wa ndoa. Mwanzo 2:18 inatuonyesha kuwa Mungu aliumba ndoa na ana mpango na kusudi nayo.

> Bwana Mungu akasema, "Si vema huyu mtu awe peke yake; Nitamfanya msaidizi wa kufanana naye." (Mwanzo 2:18)

Kwanza, kumbuka ni nani anayezungumza: "Bwana Mungu alisema." Halikua wazo la Adamu kujipatia mke; Lilikuwa ni wazo Mungu. Pili, angalia ni kipi Mungu alichosema, "Si vyema mtu awe peke yake."

Kila kitu kingine katika uumbaji wa Mungu kilikuwa kizuri (Mwanzo 1: 4, 10, 12, 18, 21, 25), lakini mtu kuwa peke yake haikuwa nzuri. Hii inaonyesha moja kwa moja kutokukamilika kwa mwanadamu. Tatu, angalia jinsi Mungu anavyosema, "nitamfanya msaidizi wa kufanana naye." Mungu alimuumba mwanamke kulingana na muundo wake, mpango wake, mawazo yake na njia zake. John MacArthur Jr. husaidia kusadikisha hatua hii kwenye familia:

> Kwa kuona hali ya mwanadamu kuwa sio nzuri, yeye (Mungu) alikuwa akitoa maoni juu ya kutokamilika kwake kabla ya mwisho wa siku ya sita kwa sababu mwanamke, mwenza wa Adamu, alikuwa bado hajaumbwa. Maneno ya mstari huo yanasisitiza hitaji la mwanadamu la mwenza, msaidizi, na wa kufanana (maana yake ni sawa na thamani ya Mungu). Hakuwa amekamilika bila mtu wa kumsaidia katika kutimiza kazi ya kujaza, kuzidisha, na kuchukua utawala juu ya dunia. [3]

Jambo muhimu hapa ni kwamba Mungu aliumba ndoa ili kutimiza mapenzi yake, sio yetu. Adamu na Hawa, kupitia uhusiano wao, wangekuwa wenzi wa kwanza kufanikisha mpango wake wa ndoa. "Bwana ni mwadilifu katika njia zake zote, ni mwenye neema katika kazi zake zote" (Zaburi 145: 17). Mungu aliumba ndoa kama kitu kizuri kwetu; lazima tuikumbatie ndoa kama zawadi ya neema kutoka kwake. Kitu ambacho watu wengi wanashindwa kutambua ni kwamba Mungu aliumba ndoa kwa *faida* yetu kwa kuwa Mungu ni mwadilifu. Itakuwa sio haki ikiwa angekupa kitu muhimu kama ndoa bila maagizo ya wazi na nguvu ya Roho Mtakatifu kukuwezesha kumheshimu ili kufaulu.

Kwa bahati mbaya, hata wengi wanaojiita waamini, wamekuwa wakiuacha ukweli siku kwa siku. Wengi wanaodai kuwa Wakristo leo hawaamini kuwa Biblia ni muhimu kwa maagizo juu ya ndoa au malezi. Katika ushauri na saha, ukweli huo unajidhihirisha sana. Wengi ambao wamekuwa Wakristo kwa miaka mingi hawajui kanuni za msingi za kibiblia katika ndoa.

Hii inaonyesha kuwa hawana maaarifa ya juu ya Biblia au hawajaambiwa kwamba taarifa wanayohitaji iko katika Biblia. Kwa namna yoyote, hawajui ya kwamba Maandiko yanaweza kusababisha uelewa na kufunua jinsi ndoa inavyopaswa kufanya kazi.

**Kujichunguza 1**

Muombe Mungu afunue mtazamo wako wa kweli kwa Neno lake. Andika maombi kwa imani ya kumtumaini, kuamini yote atakayoonyesha juu ya ndoa kutoka katika Neno.

Ukweli ni kwamba, kwa kuwa mwenzi wako ni zawadi kutoka kwa Mungu, na ana upendo mkubwa kwao kuliko wewe, lazima tuamini kwamba yeye hutoa kila kitu unachohitajika kujua juu ya kuwatunza. Anataka matendo yako yamtukuze na yambariki mwenzi aliyekupa.

**Mtazamo Bora juu ya Neno la Mungu**

Ni muhimu kwako kujua kwamba Neno la Mungu ni kweli na kwamba yeye hutoa majibu yote kwa maisha ya kimungu na ndoa yenye mafanikio. Tulijifunza katika somo la 1 kwamba tuna "nguvu ya kimungu", na yeye "ametupatia vitu vyote vinavyohusiana na uzima na utauwa" (2 Petro 1: 3-4). Mungu hutumia Neno lake, ambalo "lina uhai na nguvu" (Waebrania 4:12), kutubadilisha. Kama vile Paulo alivyomwandikia Timotheo, alimtia moyo alitegemee kabisa Neno ili kuwaongoza na kuwabadilisha wale walio katika kanisa alilokuwa akilichunga. Lazima tuwe na mtazamo huu huo. Neno la Mungu "lina faida" kwa kuongoza na kurekebisha tabia zetu (2 Timotheo 3:16).

Tafakari juu ya Maandiko yafuatayo:

> Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, layafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo njema. (2 Timotheo 3: 16-17)

**Kujichunguza 2**

Tambua jinsi mstari hii inavyotumika kwa kujifunzia na jinsi inavyoweza kusaidia ndoa yako ikiwa utaitumia.

______________________________________________
____________________

______________________________________________
____________________

______________________________________________
____________________

______________________________________________
____________________

______________________________________________
____________________

______________________________________________
____________________

______________________________________________
____________________

Je! Mistari hii inaelezeaje mtazamo mzuri juu ya Neno la Mungu? Je! Unaamini ni ukweli? Je! Unali karibisha?

**FAILI LENYE UKWELI**

*Mafundisho* -Maagizo ya kimungu au ya Mungu hutoa mwongozo kamili na ukweli wa kimungu unaohitajika kwenye maisha, utauwa, na familia.

*Kukemea* -Neno la Mungu linatuambia kile kibaya au dhambi katika imani na tabia.

*Marekebisho* -Neno la Mungu linatuambia jinsi ya kurudisha kitu katika hali yake inayofaa, kuweka sawa kitu kilichoanguka, kinachoonyesha maisha ya kimungu.

*Maagizo katika haki* - Maandiko hutoa mafunzo mazuri (*mafundisho* hapo awali yalitajwa kumfundisha mtoto) katika tabia ya kimungu, sio kukemea tu na kurekebisha tabia mbaya (Matendo 20:32; 1 Timotheo 4: 6; 1 Petro 2: 1, 2). [4]

Limetolewa kwa ajili ya kazi njema-Lengo la Mungu ni sisi kuyaelewa mapenzi yake na kuwa tayari kuatenda kwa kufuata kanuni zake za kibiblia

Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu katika kutakaswa na roho na kuimanika kweli (1Wathethalonike 2:13).

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua njia sahihi na zisizo sahihi katika kupokea Neno la Mungu kwa sifa za kila mmoja.

> Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa msikiliaji wa neno tu, na wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayeangalia uso wake kwenye kioo; maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru na kukaa humo, asiwe msikiliaji msahaulifu bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake. (Yakobo 1: 22-25)

Tunapaswa kuwa na mtazamo gani kuhusu Neno la Mungu?

Je! Ni yapi matokeo mazuri tunapolitii Neno la Mungu?

Tambua nini ambacho kifungu hiki kinasema juu yako na Neno la Mungu.

> Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na meneno yote yaliyoandikwa humo. Maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapostawi sana. (Yoshua 1: 8)

Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiburudisha nafsi.
Ushuhuda wa Bwana ni amini, humtia mjinga hekima.
Maagizo ya BWANA ni ya adili, huufurahisha moyo.
Amri ya Bwana ni safi, huyatia macho nuru.
Kicho cha Bwana ni kitaktifu, kinadumu milele.
Hukumu za Bwana ni kweli, zina haki kabisa.
Ni za kutamanika dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi;
Nazo ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali.
Tena mtumishi wako huonywa kwazo, katika kuzishika kuna thawabu nyingi.
(Zaburi 19: 7-11)

Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa safi ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu. Ikiwa mmeonja ya kuwa Bwana ni mwenye fadhili. (1 Petro 2: 2–3)

**Kujichunguza 3**

Je! Una uhakika wakati huu katika safari yako ya ndoa kwamba unajua jinsi ya kumhudumia mwenzi wako kulingana na Neno la Mungu? ___ Ndio/Hapana

Mungu anajua nguvu na udhaifu wako na anaahidi kukupa hekima na nguvu ikiwa utatafuta na kutamani kutenda mapenzi yake katika ndoa yako. Andika mawazo machache ukimwambia Mungu jinsi unavyoshukuru kwa ahadi hii.

**CHIMBA ZAIDI**

Paulo aliweka nia yake katika kumpendeza Mungu. Alikuwa na malengo makubwa juu ya hilo.

> Kwa hivyo basi ikiwa tupo hapa au ikiwa hatupo hapa twajitahidi kumpendeza yeye. (2 Wakorintho 5: 9)

Andika maombi ukimwambia Mungu kuwa una lengo la kumpendeza kwa kukamilisha kitabu hiki.

## Somo la 4

## Dhumuni la Mungu kuhusu Ndoa

Katika mpango wa Mungu wa ndoa, ametupa madhumuni muhimu, au sifa, ambazo lazima tuzizingatie ili kutimiza mapenzi yake. Kanuni za kibiblia hapa chini zitaweka mbinu za kutumia kitabu hiki cha kujifunzia. Mbinu hizi zitatajwa mara nyingi na ni muhimu kwa ndoa yenye mafanikio.

### Huduma ya Ndoa

Tunaposikia neno *mtumishi*, kwa kawaida tunafikiria mchungaji au mtu anayefanya kazi kanisani. Lakini, neno hili lina maana nyingine.

Je! Hili linajitokezaje kwenye ndoa zetu za Kikristo? Tuko chini ya uangalizi na mamlaka ya Yesu Kristo, ambaye ni nafsi moja na Mungu Baba na tunapokea maagizo kutoka kwake. Mungu ametupa wenzi wetu wa ndoa na anatamani tutende mapenzi yake kwao kwajili yao. Sisi ni *watumishi* wa wenzi wetu, chini ya Mungu. Mawazo haya yatabadilisha kabisa tabia yako na mtazamo wako juu ya ndoa.

Je! Umeona jukumu lako kama la Mtumishi?
___ Ndio/Hapana

**FAILI LENYE UKWELI**

*Huduma* (nomino)-*Diakonos*(Kigiriki). Mtumishi au mhudumu, yule anayesimamia, anatawala, na anatimiza.

*Hudumia* (kitenzi) -Kurekebisha, kusahihisha na kuweka utaratibu; kutumikia, kutoa huduma kwa mwingine; kufanya kazi kwa Bwana kama mtumishi. Muhudumu ni yule anayetenda chini ya amri ya mwingine, au ambaye yuko chini ya mwingine kutekeleza malengo yake. Kama Wakristo sisi tuko chini ya Yesu. Na kama watoto wake tuko hapa kutimiza mapenzi yake.

Katika ndoa, kumtegemea kabisa Bwana Yesu Kristo ni suala muhimu.

Hatupaswi kutukuza mapenzi na matakwa yetu wenyewe, lakini tunawajibika kufuata mapenzi ya Bwana na shauku yake katika uhusiano wetu wa ndoa. Mathayo 20:28 (SUV) inasema, "Kama vile Mwana wa Admu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika na kutoa nafsi yake iwe fidia kwa wengi." Ni wazi kwamba, *kuhudumia* na *kutumikia* ni sawa na Yesu ni mfano wetu katika. Usije ukakosea kwa kuchukila neno *kuwahudumia* kwa mtazamo wa kidunia pengine kwa kumdekeza sana mke wako, bali tumika kwa kumpenda na kumchunga kulingana na maelekezo ya Mungu. Tunapoanza kuona ndoa zetu kama kumtumikia Mungu na kuwahudumia wenzi wetu kwa madhumuni yake, tunaanza kuelekea katika mwelekeo sahihi.

Kwa kuwa Mungu aliumba mwanamume, mwanamke, na ndoa, tunapaswa kutekeleza makusudi yake katika umoja huo mtakatifu. Mungu amewafanya waume na wake kutimiza mapenzi yake kwa kila mmoja. Ili ujione mwenyewe katika jukumu hilo, kama mtumishi chini ya Mungu na chini ya mpango wake kwako; basi tumika, ni muhimu sana. Ikiwa una mtazamo wa Mungu kama mtumishi, basi hautakuwa ukibishana au kusisitiza mapenzi yako mwenyewe, ukipigania kupata kile unachotaka. Ikiwa ninyi wawili mna shauku ya kutimiza mapenzi ya Mungu, kama watumishi wake kwa kila mmoja, mtakuwa baraka na kutiana moyo kwa kila mmoja.

Andika maombi ukimwomba Mungu akusaidie kujiona kama Mtumishi kwa mwenzi wako kama huduma yako ya kwanza.

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

**CHIMBA ZAIDI**

Eleza jinsi Paulo na wenzake walivyowahudumia watu. Walionyesha mitazamo gani?

> Bali tulikuwa wapole katikati yenu, kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe. Vivyo hivyo nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tuliona furaha kuwapa; si Injili ya Mungu tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu. (1 Wathesalonike 2: 7-8)

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

________________________________________________________________________
____________________________________________

**Mwongozo wa Haki**

Kama watumishi wa Mungu lazima tujue nia Zake, kile Anachotaka tukamilishe, jinsi ya kuendelea, na jinsi ya kutumikia wale anaotupatia. Kuelewa madhumuni Yake pia hutusaidia kukumbuka hitaji letu la kila siku la hekima na nguvu za Mungu.

> **FAILI LENYE KWELI**
>
> *Kusudi* - Matokeo au lengo lililokusudiwa, au linalotarajiwa.

Wanandoa wa Kikristo wanapoulizwa katika ushauri jinsi wanaona kuwa watumishi kwa wenzi wao, wanatoa majibu mengi tofauti. Ni dalili ya ukosefu wa umoja kati ya waume na wake katika eneo hili. Kwa kiwango fulani, hii ndio shida kuu: watu wawili walio na jukumu moja wanapoenda pande mbili tofauti, kuchanganyana na mionekano hasi mingi inaweza ikatokea. Biblia inatuonyesha kuwa huu sio mpango wa Mungu.

> Kwa maana Mungu sio machafuko bali wa amani. (1 Wakorintho 14:33)

Cha kusikitisha ni kwamba, mwili wa Kristo haujatoa upendeleo wa kufundisha au kutokufundisha watu katika ndoa. Makanisa mengi hayajawahi kukuza utumishi wa ndoa au kuanzisha darasa juu ya maagizo ya Mungu kuhusu ndoa; ingawa makanisa yamejaa watu wanaotafuta ushauri juu ya ndoa. Wakati wa ujana wetu, tunapata mafunzo kwa masaa hamsini au zaidi ili kupata leseni za udereva, lakini ni masaa ngapi ya mafunzo yanahitajika ili kuoa? Hakuna. Kwa sababu ya ukosefu wa mafunzo, wenzi wengi, hata wenzi wa Kikristo, wanaweza kuwa na ushawishi mbaya sana kwa kila mmoja.

Wakati mume na mke wanapokuwa hawakubaliani na hawaeleweki katika malengo yao waliyopewa na Mungu, hapo ndipo shida huibuka, ikifuatiwa na mvutano, ugomvi na mgawanyiko. Shida hii juu ya ndoa na familia zao ni shida kubwa inayoishi katika mwili wa Kristo leo.

Katika Mathayo, Yesu alifunua ukweli unaojidhihirisha:

> Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa, na kila mji … hatasimama. (Mathayo 12:25)

**Kujichunguza 1**

Andika sala. Muombe Mungu, kama mume na mke, akupe neema ya kuanza upya katika ndoa yako. Muombeni rehema ya kusameheana katika makosa ya zamani na kwa kutofanya kazi kwa usawa na mwombeni afungue mioyo yenu ili muweze kupokea maagizo yake ya kufanya kazi pamoja kama timu.

Tafakari juu ya mitazamo ambayo Mungu anataka juu yetu.

> Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu mpendwao, jivikieni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole na uvumilivu, mkichukuliana na kusameheana. Mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo nanyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo ndiyo kifungo cha ukamilifu. Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu, ndiyo mlioitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani. Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na nyimbo za kiroho, huku mkimwimbia Bwana kwa neema mioyoni mwenu. (Wakolosai 3: 12-16)

Msingi wa yote tunayofanya lazima uwe uelewa wa madhumuni na mipango ambayo Mungu anayo kwetu. Mara tu tunapokubali mamlaka ya Mungu, ni muhimu kufuata kwa njia za vitendo. Mungu ndiye mhandisi, lakini ni kazi yetu kujenga nyumba kulingana na ramani yake. Tunapokielewa kile ambacho Mungu anajaribu kufanya kupitia sisi na ndani yetu, wakati tunafuata mpango wake, basi tunajua kwanini ni muhimu sana kuwa na uhusiano mzuri na Kristo.

**CHIMBA ZAIDI**

Elewa jinsi mstari huu unavyohusiana na wewe kama mwenzi na mhudumu.

> Kwa maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo. (Waefeso 2:10)

______________________________________________________________________
_______________________________________________

______________________________________________________________________
_______________________________________________

______________________________________________________________________
_______________________________________________

**Dhumuni la nne**

Kusudi la Mungu kwetu kama wenzi wa ndoa na wahudumu linaweza kugawanyika katika maeneo manne:

1. Anataka kutukuzwa katika uhusiano wetu.
2. Anataka tubadilishwe tuwe na mwonekano wa Kristo.
3. Anataka sisi kukidhi mahitaji ya urafiki wa kila mmoja.
4. Anataka tuwalee watoto wetu kulingana na Neno lake.

**Kusudi la Kwanza: Utukuzwaji wa Mungu**

Kusudi letu kuu kama waamini ni kumtukuza Mungu. Wakorintho wa Kwanza 6:20 inasema, "Kwa maana mlinunuliwa kwa bei; kwa hiyo mtukuzeni Mungu katika miili yenu na kwa roho zenu, ambazo ni za Mungu." Neno *kutukuza* linamaanisha "kuakisi." Kama waamini na wahudumu wa Mungu kwa wenzi wetu, tunapaswa kutenda kwa mfano wake kwa wenza wetu.

**FAILI LENYE KWELI**

*Tukuza* -Kutafakari, kuheshimu, kusifu, kutoa heshima au heshima kwa kumweka katika nafasi ya heshima. [5]

> Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuza Baba yenu aliye mbinguni. (Mathayo 5:16)

Yesu alikuwa anasema, "Nataka uonekane kama mimi, kumtukuza Baba aliye mbinguni." Katika ndoa yako, ni mara ngapi mwenzi wako anaona mwangaza wa Mungu katika nafasi au tabia yako? Je! Unajali kuhusu hilo kila siku? Fikiria jinsi kanuni hii moja tu ya kibiblia inavyoweza kubadilisha uhusiano wako ikiwa kila asubuhi ungeomba, "Mungu, ninataka mwenzi wangu akuone kwa jinsi ninavyotenda na kujibu kwa sababu shauku yako ni kutukuzwa ndani yangu."

Kumbuka, Mungu anatubadilisha kutoka ndani, hali ambayo inadhihirika kwa matendo na tabia zetu. Mabadiliko yetu huwa halisi tunapoonyesha asili ya Kristo kwa wale walio karibu nasi.

**Kujichunguza 2**

Tambua maneno, mitazamo, na tabia unazoonyesha kwa mwenzi wako ambazo hazimwakisi Mungu.

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

Waume, Waefeso 5:25 inasema, "Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama vile Kristo pia alivyolipenda kanisa na akajitoa mwenyewe kwa ajili yake." Hii inamjulisha mwanaume kwamba; mawazo yake, maneno na matendo kwa mkewe yanapaswa kuonekana kama matendo ya Yesu kwa Kanisa. Hili ni jukumu kubwa ambalo ametuwekea. Hatuwezi kufanya hivi kwa nguvu zetu wenyewe – tu bali kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu.

Wake, Waefeso 5:22 inasema, "Wake, watiini waume zenu, kama kwa Bwana," mkimwambia mke kwamba anapaswa kumtendea mumewe vile vile anavyomtendea Bwana.

***MPANGO KAZI***

Orodhesha matukio yoyote katika wiki iliyopita ambayo umemwakilisha Mungu vibaya. Omba Mungu akusamehe, halafu nenda kwa mwenzi wako na ufanye vivyo hivyo. Usitoe sababu.

**Kusudi la Pili: Mabadiliko yetu**

Je! Sio vyema kujua kwamba Yesu Kristo alikuita kwake mwenyewe, hakusema, "Nenda ukasafishwe, acha kufanya mambo yako yote mabaya, kisha urudi nione kama nitakukukubali." Wakati Mungu alituita kwake, alituchukua jinsi tulivyokuwa. Tumsifu Bwana!

Mungu aliponikamata, nilikuwa nikikimbia kilometa mia kwa saa kuelekea upande mwingine, lakini jambo la kushangaza kwenye suala langu la kuzaliwa mara ya pili ni pale Bwana alipogusa akili na moyo wangu na maneno, "Ninakupenda, na ninakutaka." Nilijiuliza *ananitaka kivipi*. Katika hali yangu ya dhambi, ilikuwa upendo wake ambao ulinilazimisha kumpokea na kumwomba awe Bwana na Mwokozi wangu. Hata hivyo, hakutaka nibaki katika maisha yangu ya ubinafsi na dhambi. Mungu aliuteka moyo wangu na akanionyesha mtazamo wake kwa maisha yangu.

Sikujui wewe, lakini najua wewe ni mbaya. Nakuhakikishia wewe ni mwenye dhambi (Warumi 3:23). Tunakuja kwa Kristo tukiwa bado tunatenda dhambi (Warumi 5: 8), "bila nguvu" mstari 6), na "maadui" wa Mungu (mstari 10). Lakini Mungu anasema kwamba tangu wakati wewe na mimi tunapomkubali Kristo, safari ya mabadiliko, au kile ambacho Biblia inaita utakaso (1 Wakorintho 1:30), huanza. Wewe na mimi tunapaswa kuweza kutazama nyuma na kusema tunaonekana kama Yesu leo kuliko jana. Hata hivyo, Wakristo wengi hawajui jinsi mchakato wa Mungu na utakaso hufanya kazi ndani ya ndoa. Kubadilishwa kuwa mfano wa Kristo ni mpango na kusudi la Mungu kwa kila mwamini.

Mtume Yohana alitupa himizo ambalo linaunganisha utunzaji wa Neno la Mungu na kukamilishwa au kuwa wakomavu.

> Lakini yeye ashikae neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake. (1 Yohana 2: 5)

Maneno "hushika Neno lake" inamaanisha kujua Neno lake na kulifanya, na kisha "upendo wa Mungu umekamilika" ndani yetu.

> Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu, kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake. (Yohana 15:10)

**FAILI LENYE UKWELI**
Kukamilika- *Teleio (Kigiriki),* kutimilika, jambo ambalo liko katika mchakato hasa wa kumalizika, kufikia lengo lililokusudiwa au kumaliza kazi

Tunapojua Neno lake na tunatamani kulishika, tunapata mabadiliko ndani yetu na matokeo yake hujionyesha katika tabia zetu. Katika hali za kila siku, zikiwemo changamoto za maisha katika familia, Mungu huwaumia wenzi wetu katika kufunua mambo ambayo yamo ndani yetu naye huyachukia; yaani tabia za dhambi na mitazamo katika mahusiano yetu.

Je! Uliwahi kufikiria kwamba mwenzi wako hutumiwa na Mungu kukugeuza kuwa mfano wa Kristo? Tunaposema au kufanya jambo lisilo la kumcha Mungu, tunasema, "Umenifanya nitende hivi." Lakini hatuwezi kupata hiyo katika Neno la Mungu. Mungu anasema, "Kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake" (Mathayo 12:34). Uovu huo huwa ndani na Mungu anatumia mwenzi wako kuutoa na kukuonyesha kile kinachohitaji kubadilika. Tunapodai kutokuwa na hatia au kuwalaumu, tunashindwa kuwajibika. Ni muhimu sisi kama watumishi tuelewe kwamba Mungu anatumia mienendo ya familia zetu kutusafisha na kutubadilisha kuwa mfano wa Kristo.

> Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo tutabadilishwa tufanane na mfano huo huo toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa Roho wa Bwana. (2 Wakorintho 3:18)

Vivyo hivyo Mkristo hubadilishwa pole pole kuwa mfano wa Kristo na anakuja kutamani mapenzi ya Mungu katika vitu vyote.

**FAILI LENYE UKWELI**
Badilisha-*Metamorpho o(*Kigiriki) ni kubadilika na kuwa kitu tofauti kabisa. Mfano kiwavi kuwa kipepeo.

**Kujichunguza 3**

Mstari unatuhakikishia kwamba Mungu yuko kazini akikubadilisha. Je! Unaweza kumtumaini na kumwomba afunue maeneo ambayo bado unahitaji kuboreshwa? ___ Ndio/Hapana

Andika nia ya kujitolea kwa ajili ya maombi, kukubali njia yake kamili ya kufunua ukosefu wako wa kufanana na Kristo.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua kile ambacho Mungu anaahidi kufanya ndani yako.

> Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu. (Wafilipi 1: 6)

________________________________________________________________________
_______________________________________________

________________________________________________________________________
_______________________________________________

________________________________________________________________________
_______________________________________________

Kazi hii nzuri ni mchakato wa kufanana na Kristo, katika hali ya kukufanya kuwa mtumishi wake na mwenzi anayetaka wewe uwe.

Je! Bado unayo nafasi ya kukua katika eneo hili? ___ Ndio/Hapana

Lazima tujihakikishe mioyoni mwetu kwamba Mungu hutumia tofauti kati ya waume na wake kama nyenzo za kujifunzia utii juu mapenzi yake. Wakristo wengi hukataa ukweli huu kwa sababu ya ujinga wao, bila kutambua kwamba hii ni sehemu ya mchakato wa utakaso. Ndoa ni sehemu ya kambi ya mafunzo ya Mungu.

Majaribu mengi tunayokabiliana nayo yeye ndo alie yaumba. Mungu huruhusu mambo magumu na zaidi huruhusu pia utende dhambi (isiyo ya kufanana na Kristo). Elewa kwamba alipanga hali hii kudhihirisha mambo haya ndani yako, sio ili umlaumu mwenzi wako, bali usema, "Ee, Bwana wangu, hali hii ilikuwepo pindi uliponikubali na unaitumia sasa katika kufunua dhambi yangu ili niweze kutubu na kuacha kuifanya tena. ”

Mungu haruhusu hali hizi ili aweze kujua kilicho ndani yetu. Tayari anajua na anaona yote na bado anatupenda.
Anafanya hivyo ili tujione na kutamani msaada wake na tubadilike.

> …kwa fedha, na tanuru kwa dhahabu; Bali
> Bwana huijaribu mioyo. (Mithali 17: 3)

**Kujichunguza 4**

Majaribu haya yanapokuja, je! Ni mitazamo na matendo gani yasiyo ya kimungu yanayojidhihirisha kwako kupitia mwenzi wako au watoto?

________________________________________________________________________
_______________________________________________

________________________________________________________________________
_______________________________________________

________________________________________________________________________
_______________________________________________

________________________________________________________________________
_______________________________________________

Tafakari kile ambacho Mungu anafanya ndani yako kupitia mistari hii.

> Tazama, nimekusafisha, lakini si kama fedha;
> Nimekuchagua katika tanuru ya mateso. (Isaya 48:10)

> Mimi, Bwana, natafuta moyo,
> navijaribu viuno,
> Hata kumpa kila mtu kiasi cha njia zake, kiasi cha
> matunda ya matendo yake. (Yeremia 17:10)

Dhumuni la tatu na la nne yamefunikwa katika somo linalofuata.

## Somo la 5

## Kukubaliana na Nidhamu ya Mungu

Tunapowajibika (umiliki) kwa sababu ya tabia zetu, tunapaswa kumwomba Mungu na wenzi wetu watusamehe na kumuomba, "Mungu, ondoa hiki ndani yangu." Hapo ndipo mabadiliko yanapoanzia. Pasipo kupitia hatua hii, hatuwezi kukua. Mara nyingi wanandoa wa Kikristo wanapoingia kwenye ushauri na saha pengine wanakuwa na miaka mitano, kumi, hata ishirini ya mawasiliano yenye sumu nyuma yao, kwa sababu hawakuelewa mapenzi ya Mungu katika eneo hili; hufika wakiwa wanahisi kutokuwa na tumaini na waliokata tamaa kabisa.

Hata baada ya kujifunza kuwa Mungu hutumia uhusiano wetu kama mume na mke ili kutubadilisha, mbali na neema yake ya kila siku, hatuwezi kumpokea na kushirikiana naye katika eneo hili. Tunapokuwa hatuiishi ndani ya Kristo kila siku na majaribu yanapotokea, pengine tunachukua hatua za kibinadamu kwa hasira, kiburi, lawama, kujionea huruma, na mengine mengi. Inazidi kuwa kawaida kwa Wakristo kuamini kwamba tabia zao za dhambi ni matokeo ya sababu za nje, kwa hiyo wao sio wa kulaumiwa. Tukiwa tunakaa ndani ya Yesu kila siku, tukimtazamia yeye kwa neema na kuyatenda mapenzi yake, hapo ndipo tutaweza kupata mabadiliko ya ndani.

> Tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahmili msalaba, na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. (Waebrania 12: 2)

**Kujichunguza 1**

Yesu "alivumilia" maumivu ya msalaba kwa sababu ya matokeo ya furaha, na wokovu wa roho zetu. Je! Ni furaha gani unayoona ambayo hufanya maumivu ya mabadiliko yafae? Taja angalau maeneo mawili ambayo Mungu anafunua ndani yako ambayo anataka kuyabadilisha (hasira, kutokuwa na subira, chuki, kutosamehe, ukali, uchungu, kukwepa, n.k.).

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Mstari huo pia unasema, "Kumtazama Yesu." Andika maombi ya kujitolea kumtazama yeye wakati suala lenye changamoto ya ndoa linapokuja nyumbani kwako.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

Mara kwa mara Mungu hutumia vitu ambavyo tunaviona kuwa sio vya haki katika kufanya kazi yake. Je! Umewahi kusoma hadithi ya Yusufu? Huyu ni kijana ambaye kwa miaka ishirini na tano angekuwa katika tiba. Angeweza kuwa kwenye kila utabiri ijulikanayo duniani leo. Kaka zake walikuwa na wivu. Kwa hivyo wakampiga, wakachimba shimo ardhini na kumtupa huko walitaka afie huko. Baadaye wakabadilisha mawazo yao na kumuuza kuwa utumwa (kana kwamba hiyo ilikuwa bora).

Maisha ya Yusufu yalikuwa yameharibika, lakini hakuwa hivyo, kwa sababu aliweka imani yake na kumtegemea Bwana. Baadaye Yusufu alikutana na ndugu zake, na waliumia sana kwa sababu ya kile walichomtendea. Mwitikio wake ulikuwa, "Mlikusudia, mabaya juu yangu; lakini Mungu alikusudia mema, ili kunifanya kama nilivyo leo, kuwaokoa watu wengi waishi"(Mwanzo 50:20). Yusufu alikuwa na kila sababu maishani mwake za kusema, "Mungu, maisha yananuka, hayana haki, na nitafanya tu ninachotaka." Soma hadithi yake katika Mwanzo 37-50 kuhusu jinsi alivyomwamini Mungu.

Hata hivyo, kama Wakristo leo, ikiwa mwenzi wetu anatukatisha tamaa au kukatisha tamaa, inatarajiwa kuwau, tutakasirika na kutenda dhambi. Wakati wote Mungu anasubiri mwangaza uendelee, kwa sisi kutambua kuwa yeye anaruhusu majaribu kwa faida yetu. Ingawa Mungu hatuhukumu au hana lolote la kufurahishwa nalo katika dhambi, yeye hataki tusamehe dhambi zetu na kukaa katika hali ya kutotii. Sehemu ngumu zaidi kwetu ni pale Mungu anapofungua vidole vyake kutuzunguka wewe na mimi na kuanza kutuumba upya kwa matengenezo; hii huweza kutuumiza. Biblia inasema, "Yeye ndiye mfinyanzi" na sisi ni "udongo."

> Je! Unaweza kuwa mpumbavu kiasi gani?
> Yeye ndiye Mfinyanzi, na hakika yeye ni mkuu kuliko wewe, udongo! Je!
> Kitu kilichoumbwa kinapaswa kusema juu ya yule aliye kiumba,
> "Hakuni tengeneza mimi?’’
> Kikombe kishawahi kusema,
> "Mfinyanzi aliyenifanya mimi ni mjinga"? (Isaya 29:16)

Mara nyingi katika mazingira ambayo tunakuwa tumeumizwa, Mungu akiwa anajaribu kuleta mabadiliko, huwa tunamwambia, “Ondoa mkono wako juu yangu, Bwana! Sitaki kutengenezwa na wewe. Sipendi jinsi unavyofunua asili yangu ya dhambi na kunifundisha! ” Ni jambo la kijinga sana kusema kwa Muumba wetu.

Labda haujamwona mume wako au mke wako kama vidole vya Mungu, lakini anayokwambia ni kweli. Ataendelea kutushinikiza mpaka tujisalimishe au tujishushe. Watu wengi walioolewa hawana furaha sana, hawaoni kitu ambacho Mungu anataka, kwa sababu hawajui kusudi lake kwenye ndoa zao.

Bwana amemtumia mke wangu kufunua vitu ndani yangu ambavyo sikuvipenda na najua Mungu hakuvipenda pia. Amemtumia mtoto wangu wa kwanza Nick kuliko kitu chochote au mtu yeyote duniani kufunua ubaya ndani yangu. Sikujua ni jinsi gani nilikuwa na hasira ndani mpaka mtoto wangu alipokuja. Alipokuwa na umri wa miaka mitatu, aliweza kunikasirisha kuliko mwanadamu mwingine yeyote hapa duniani. Lakini, Mungu alinifunulia, "Sio Nick, Craig, ni Mimi, mimi ndiye niliyemweka mtoto huyu mwenye mapenzi makuu maishani mwako kufunulia vitu ninavyochukia ndani yako. Ninapovifunua na ukiniomba nikubadilishe, hautabadilika kamwe mpaka ukubali kuwa ni wewe na utubu. Na hautakuwa na uhusiano na mtoto wako pia. Ni juu yako, Craig. Jisalimishe au uteseke. ”

Hatupendi changamoto au mateso. Wakristo wengi wanafikiria, "Loo, subiri kidogo, Mungu, ninapaswa kuwa na furaha." Ndio, lakini sio kwa njia yako, kwa sababu tuna ubinafsi. Mimi na wewe hatupaswi kumwambia Mungu, “Sawa, najua ninachohitaji. Hii ndio orodha yangu. ” Mungu anajua sisi ni waovu. Neno lake linasema hatuwezi kuamini mioyo yetu wenyewe. Lazima tuangalie Neno la Mungu. Yesu alisema katika Yohana 6:38, "Kwa maana nimeshuka kutoka mbinguni, si kufanya mapenzi yangu mwenyewe, bali mapenzi ya yeye aliyenipeleka." Kumtukuza Mungu kunamaanisha kuishi mapenzi yake na kusudi lake katika na kupitia maisha yetu.

**Kusudi la Tatu: Kukutana na Mahitaji ya Urafiki**

Kusudi linalofuata ni kukidhi mahitaji ya urafiki wa kila mmoja (Mwanzo 2:24). Tena, hii haikamiliki kwa njia yetu wenyewe au kwa nguvu zetu, lakini kwa Neno na neema yake. Lazima tuelewe na tuamini kwamba Mungu alimuumba Adamu na kisha Hawa kama "msaidizi anayefanana naye."

> Mungu alisema, “Si vema mtu huyu awe peke yake; Nitamfanya msaidizi wa kufanana naye.” (Mwanzo 2:18)

Mungu anahitaji ndoa ya mwanamke na mwanaume kuwa kitu kimoja na siyo kitu kinachoendana, bali muungano huo wa wawili ulete umoja uliokamili. Sitakiwi kuwa kama mke wangu ama mke wangu kuwa kama mimi, la bali Mungu anataka kila mmoja awe akubaliane na upekee wa mwenzake na kuwa jozi zinazofanana ili kukidhi mahitaji ya urafiki wa kila mmoja wetu; kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu. Anataka sisi tuwahudumie wenzi wetu, kushirikiana nao na kuunda uhusiano na urafiki wa kudumu.

Kulingana na maelezo haya katika Kitabu cha Mwanzo, kwa kuona kuwa haikuwa sawa kwa mtu huyo kuwa peke yake, Mungu alimpa msaidizi. Angalia neno alilotumia hapa ni *msaidizi*, sio kiongozi au kocha. Mungu alimuumba mwanamume kutoka kwa mavumbi ya ardhi (Mwanzo 2: 7), lakini pia aliunda — kwa tafsiri ya neno kwa neo akatengeneza - mwanamke kutoka kwenye ubavu wa mwanamume (Mwanzo 2: 21–22).
Mungu alikuwa akionyesha jukumu ambalo mume na mke wangekuwa nalo katika maisha kwa kila mmoja. Wangekuwa wanategemeana.

yaani, mtu huyo alihitaji ushirika na msaada. Mungu alitoa msaada huo kupitia mwanamke. Mwanamke atakidhi kile kilichokuwa kinakosekana kwa mwanamume, na kinyume chake. Uhai wa mwanamke ulitoka kwa mwanamume na maisha ya mwanamume yangetoka kwa mwanamke.

**Kujichunguza 2**

Mke, je! Unataka kuwa msaidizi / msaada kwa mumeo? ___ Ndio ___ Hapana (Mwambie sasa.)

Waume, mko tayari kukubali mwenyewe na kwa wake zenu kuwa mnamhitaji? ___ Ndio ___ Hapana (Mwambie sasa.)

Mungu pia anatamani kwamba mume na mke wawe na uhusiano wa kipekee ambao yeye nnauita "mmoja" kiroho, kihisia na kimapenzi; na hivyo kutimiza mahitaji ya urafiki wa kila mmoja. Mungu alisema hivi tangu mwanzo.

> Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake na ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. (Mwanzo 2:24)

Katika Mathayo 19: 5-6, Yesu alisema, "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye na ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu asiwatenganishe. ”

Mungu anatamani uwe kitu kimoja na mwenzi wako. Ni vizuri sana kuwa na ukaribu sana na mumeo au mkeo kiasi kwamba unaweza kujua nini mwingine anafikiria. Je! Umepata uzoefu huo? Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka.

Mara nyingi sio lazima kumwomba chochote mke wangu kwa sababu tayari anajua kile ninahitaji, na kinyume chake.

**FAILI LENYE UKWELI**

*Kujiunga* -Kuchukua maana ya umoja wa kudumu au usioweza kufutwa, kwa hivyo talaka haikuzingatiwa. [7]

*Mwili mmoja* - umoja kamili wa sehemu zinazounda sehemu nzima. Nguzo moja, zabibu nyingi (Hesabu 13:23) au Mungu mmoja katika nafsi tatu (Kumbukumbu la Torati 6: 4); kwa hivyo muungano huu wa ndoa ulikuwa kamili na baina ya watu wawili. [8]

Tunatamani kupeana kipaumbele kwa kujua mahitaji ya kila mmoja na kukidhi mahitaji yetu kabla ya mtu kuomba chochote. Hicho ndicho ambacho Mungu anachotaka, na hii ndio siri kuu anayoizungumzia. Baada ya kuoa Mungu anapokuangalia yeye anakuona kama wawili katika mwili mmoja. Safari hapa ni kujifunza jinsi ya kutambuana na kutendeana kama vile Mungu anavyotuona, sio kujitegemea kwa kila mmoja, bali kama mwili mmoja. Wengi hawajafundishwa katika ukweli huu na bado wana mitazamo ya kujitegemea sana, ambayo inaathiri vibaya uhusiano wetu na Mungu na wenzi wetu.

Kupitia somo hili utajifunza juu ya mahitaji tofauti ya urafiki wa mume na mke. Hata hivyo, kuna hitaji moja ambalo ni sawa kwa wanaume na wanawake ambalo ni upendo. Uhitaji wetu mkubwa wa urafiki ni upendo, na Neno la Mungu hufafanua upendo wa kweli ni nini.

Mungu anawaagiza waume:

> Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyopenda Kanisa akajitoa kwa ajili yake. (Waefeso 5:25)

Mungu anawaagiza wake:

> Kadhalika ninyi wake watiini waume zenu; kusudi ikiwa wako wasioliamini Neno wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno, wakiutazama mwenendo wenu safi na wa hofu. Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani kusuka nywele na kujitia dhahabu na kuvalia mavazi; bali kwa utu wa moyoni usiionekana katika mapambo yasiyoharibika; yaani roho ya upole na utulivu iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. (1 Petro 3: 3-4)

Mungu ameweka viwango vya upendo ambavyo vinaonekana kuwa vigumu kuvitunza, lakini je! Mungu angetutaka tufanye jambo ambalo haliwezekani? Je! Mungu ni wa haki? Watu wengi wasingesema Mungu hana haki, lakini mioyo yao inasema hawawezi kuwapenda wenzi wao kama jinsi Mungu anavyotaka. Ukweli ni kwamba mtazamo huo sio sahihi kwa sisi kusema "siwezi" na zaidi "sitafanya." Huo ni uasi kwa asilimia 100. Jua kwamba Mungu aliahidi kutoa neema yake yote tunayoihitaji katika kuyatimiza mapenzi yake, ikiwa ni pamoja na kuwapenda wenzi wetu. *Amina*.

Mungu alisema natakiwa kumpenda mke wangu kama vile Kristo anavyolipenda kanisa, na mke wangu anatakiwa kunipenda kwa upendo usioweza kuharibika kama kwa Bwana. Ndio, inawezekana. Mungu si mwongo, ikiwa kasema, ni nini kitamzuia kuitimiza huduma hii ya upendo? Ni sisi tu tunaweza kuizuia, kwa sababu ya ubinafsi wetu na ukaidi au ukosefu wa imani. Kitu pekee ambacho kinaweza kuzuia hili kutimizwa ni uasi wetu.

Unapoamini kile ambacho Neno la Mungu linasema, basi ndiyo ndicho anachotaka kufanya katika na kupitia maisha yako, hapo ndipo utakapokuwa chombo chake cha kumimina upendo wake kupitia wewe. Neno la Mungu huamua thamani unayompa mwenzi wako, sio matarajio ya ubinafsi. Wakati mwenzako anaposhindwa kutii mapenzi ya Mungu, unapaswa kubaki mwaminifu katika maono ya Mungu katika ndoa. Wakati Mungu anapomwambia mwanamume ampende mkewe kama vile Kristo anavyopenda Kanisa, haimaanishi *ikiwa* anafanya kile anachokitaka yeye wakati wote. Neno lake Mungu halimwambii mke, mpende mumeo kwa upendo huu usioweza kuharibika na umheshimu kama kwa Bwana *ikiwa* tu yeye pia anafuata Neno la Mungu.

Wakristo wengi wanataka kuelekeza hasira zao na tabia zao zisizo na upendo kwa wenzi wao. Baada ya miaka kumi na tano au ishirini ya ndoa isiyofuata Neno la Mungu, ni rahisi kwao kuanzisha tabia za dhambi na kutaka kuachana. Ninawahimiza kujitolea kujifunza mapenzi ya Mungu na kuwajibika kwa chochote wanachofanya kinyume na Neno la Mungu. Kitakachotokea ni muujiza.

Ushauri wangu umekuwa msaada, lakini sio kwa sababu mimi ni mzuri. Ukweli na nguvu viko katika Neno la Mungu, sio mimi. Wakati watu wanapomuomba Mungu awabadilishe, yeye huwatendea. Wanandoa wanapokubali maneno ya Mungu, na kwa pamoja wanatamani kutenda mapenzi yake, yeye hukutana nao mahali walipo na uharibifu.

Ikiwa humwamini Mungu, unamwita mwongo; utapata matokeo mabaya, zaidi ni pale tunapokuwa na mawazo kama, *Mungu hujui tu niliyemuoa*. Tunashindwa kukiri kwamba Mungu ndiye aliyemuumba huyo mtu. Mungu anajua hali yako ni ngumu, lakini pia anajua kuwa ujinga, ukaidi, dhambi, na kutofaulu kufuata mpango wake kutaleta matokeo mabaya.

**CHIMBA ZAIDI**

Tambua mitazamo na matendo yako yanapaswa kuwa nini.

> Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba yeye huwapa thawabu wanaomtafuta kwa bidii. (Waebrania 11: 6)

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

> Hofu ya mtu huleta mtego,
> Lakini kila mtu anayemtumaini Bwana atakuwa salama. (Mithali 29:25)

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

______________________________________________________________________
____________________________________________

> Kwa maana tunaenenda kwa imani, si kwa kuona. (2 Wakorintho 5: 7)

> Maana ni kweli sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama wao;
> lakini neno lile lilolisikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu
> halikuchanganywa na imani ndani yao waliolisikia. (Waebrania 4: 2)

**Kusudi la Nne: Zidisha Kubeba Mimba na Kulea Watoto Wanaomcha Mungu**

Kuzaa sana, au kulea watoto, ni kusudi lingine lililowekwa na Mungu katika ndoa.

Mungu akamuumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba mwanamume na mwanamke alimwumba. Mungu akawabariki, Mungu akawaambia, "Zaeni mkaongezeke, mkaijaze nchi na kuitiisha…" (Mwanzo 1: 27-28)

Hiyo haina maana kwamba wenzi wote wa ndoa lazima wawe na watoto, kama ingekuwa hivyo basi watu wote wangekuwa na uwezo wa kuzaa. Kusudi moja la ndoa ni kulea na kufundisha watoto, sio kwa njia yetu bali njia ya Mungu.

Watu wengine huepuka kupata watoto kwa sababu walipitia malezi mbaya, waliumizwa, au walipata majeraha ambayo yalisababisha kutosamehe au hofu ambayo imeota mizizi mioyoni mwao. Ikiwa hii ndio sababu yako, basi mtafute Bwana ili akusaidie katika suala hilo na kukuponya. Usiruhusu dhambi za watu wengine zikunyang'anye mapenzi ya Mungu kwenye maisha yako.

Sababu nyingine ya kawaida ya kutokuwa na watoto ni ubinafsi wetu, pale tunapowachukulia watoto kama kikwazo katika mipango, matarajio, na malengo yetu. Ingawa inaweza kuwa busara kwa wenzi wengine kupanga juu ya kupata watoto baadaye ili waweze kuishi kwanza katika maisha yao mapya ya ndoa; kuhakikisha wana kipato thabiti, kumaliza shule na sababu zingine nyingi; *mpango* ukiwa ni kuishi katika utaratibu. Pia kumbuka kuwa wenzi wengi wapya wa ndoa hupata watoto mara tu wanapoingia ndani ya ndoa na wanabarikiwa kwa kuwalea. Jambo ambalo kila mwanandoa anatakiwa kulileta mbele za Bwana kwa maombi. Unapoamua kufikiri juu ya hilo, fikiria ikiwa wazazi wako wangekuwa wabinafsi na wakiwaona watoto kama kikwazo; basi wewe usingekuwa hapa.

Ikiwa unahisi hauna mbinu za kulea watoto, naomba nikutie moyo na kukutaka usome kitabu cha *Malezi ni Huduma*, ambacho kiko kwenye tovuti yetu ya FDM.world. Kama ambavyo wengi hawajafundishwa juu ya jinsi ya kuwa na ndoa ya kibiblia, vivyo hivyo huenda na katika malezi pia. Ikiwa una watoto au unapanga maisha ya baadaye, njia pekee ya kuwafanya wawe baraka kwa wote ni kuwalea kulingana na Neno la Mungu. Kwa kufanya hivyo, unamtukuza Mungu na unaweza kuwa na hakika kwamba atakupa neema na nguvu zake kutimiza kazi hii ya kushangaza.

Mimi na mke wangu tulitumia miaka yetu mitano ya kwanza kuishi katika ndoa kwa njia zetu, jambo ambalo lilisababisha kuchanganyikiwa. Mara tu tulipoamua kutumia hekima ya Mungu kulea watoto wetu, hali iligeuka kuwa ya furahi na yenye manufaa. Sasa watoto wangu ni watu wazima na naona matunda mazuri ya kufanya mambo kwa njia ya Mungu. Kwa kuongeza, tunapata maisha ya ajabu ya kuwa na wajukuu na kuona jinsi watoto wetu wanavyowalea watoto wao.

**Hakuna utani, ni Mungu!**

Je! Unahisi kuwa kutimiza makusudi ya Mungu kama mwenzi, kumtukuza Mungu kwa matendo yako yote, kukubali kubadilishwa kuwa mfano wake, kukidhi mahitaji ya urafiki wa mwenzi wako na kulea watoto ni rahisi? Sio rahisi. Ni ngumu sana.

Kutimiza madhumuni ya Mungu katika ndoa ni changamoto na inaweza kuchanganya wakati mwingine. Sio kamwe kusudi la Mungu kwetu kuogopa na kufikiria lazima tufanye hivi kwa nguvu zetu. Kwa kweli, hatuwezi kuiongoza bila yeye. Ndoa nyingi hushindwa kwa sababu hatupati na kudumisha uhusiano muhimu zaidi ambao mtu anaweza kuwa nao, uhusiano na Kristo; maana pasipo hili, hatutakuwa na ujuzi na nguvu ya kutimiza mapenzi ya Mungu.

## Somo la 6

## Msingi Imara

Mapenzi ya Mungu ni kuzibariki ndoa zetu na sisi kupata utimilifu, ingawa bado tutakabiliwa na changamoto na dhoruba katika safari hii. Kuwa na msingi imara uliojengwa juu ya Yesu Kristo ni muhimu ili kuweza kueendelea na hatimaye kushinda. Somo hili litakusaidia kuelewa jinsi ya kuwa na msingi imara wa kiroho katika maisha yako na ndoa.

Mungu aliumba ndoa, na Mungu mwenyewe amewapatia mume na mke maagizo maalum juu ya jinsi anavyotaka ndoa ifanye kazi. Maagizo hayo yanapatikana wazi katika Neno la Mungu, na ni kwa kusoma na kutii Neno lake tu ndipo tunaweza kuleta umoja, amani, upendo, na tunda la Roho katika ndoa zetu. Kuelewa na kutumia dhana hizi za kibiblia ndiyo njia pekee ya kupata baraka zote ambazo Mungu anataka uzipate ndani ya ndoa na familia yako.

Kuwa na msingi imara lazima iwe kipaumbele chako cha kwanza. Utagundua kuwa huu haukuwa mpango wa Mungu tu tangu mwanzo, katika Agano la Kale, bali pia ulikuwa ushauri wa Yesu katika Agano Jipya.

### Chaguo

Mungu anataka maagizo yake yawe wazi, kwa hivyo Maandiko mara nyingi hujumuisha mifano na kulinganisha vitu ili watu wanaweza kuelewa kwa urahisi. Katika Mathayo 7: 24-27, Yesu alielezea mfano wa wajenzi wawili: mtu mmoja aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba na mwingine aliyejenga juu ya mchanga. Hatimaye, "mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, na upepo ukavuma na kuipiga nyumba hiyo" (mstari 25). Kama ilivyotarajiwa, nyumba iliyokuwa juu ya mwamba ilibaki wakati nyumba iliyokuwa kwenye mchanga ilianguka. Yesu alikuwa akifundisha mambo mengi kwa wafuasi wake kwa muda mrefu, na mstari wa 24 unafunua hoja yake: "Kwa hivyo kila atakayesikia maneno yangu haya na kuyashika, nitamfananisha na mtu mwenye busara aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba."

Daima tuna uchaguzi wa kufuata njia ya hekima au njia ya upumbavu. Hakuna njia mbadala ya tatu. Njia moja inatuongoza kwenye mafanikio na nyingine katika kushindwa.

### Mpango wa Mbunifu

Miaka mingi iliyopita, nilikuwa mpanga ardhi ambaye alijenga maeneo ya viwanda, vituo vya ununuzi na vituo vya kuhifadhi vitu. Nilihusika katika ununuzi wa ardhi ya ujenzi wa jengo la ofisi, kulingana na uchambuzi wa gharama, palionekana kuwa na faida, lakini mkandarasi alipomaliza mipango, msingi ulikuwa mkubwa mara nne kuliko ile iliyotarajiwa na kuongeza gharama za ziada.

Mkandarasi huyo alipoulizwa alielezea kuwa kama futi thelathini chini ya ardhi hii kulikuwa na kiwango cha matope. Kwa maoni yake mtaalam, njia pekee ya kujenga salama palihitaji msingi mkubwa wa kusaidia jengo hilo. Mpaka kufikia wakati huu katika taaluma yangu, nilikuwa nimekamilisha miradi kadhaa inayochukua zaidi ya mita za mraba milioni moja; hivyo ningeweza kuchagua kufuata uzoefu wangu mwenyewe badala ya ushauri wa mkandarasi. Fikiria nini kingetokea ikiwa baada ya kupokea mpango huo name nikachagua kujenga kulingana na uzoefu wangu wa zamani.

Ikiwa nitachagua kupunguza msingi kuzingatia na kile nilichodhani kitatosha, tatizo lingakuwa kubwa kama dhoruba na matetemeko ya ardhi yangetokea, msingi ungekuwa na nyufa.

Ubovu huo ungesababisha msingi uvunjike, nyufa zingeanza kuonekana kwenye madirisha, milango ya ingefika mahali ambapo milango haiweza tena kufunga, ngazi zingeanza kupasuka, na njia za lifti zingekaa upande. Hatimaye, jengo hilo lingechukuliwa kuwa sio jengo salama kwa sababu ya msingi dhaifu na uharibifu nyufa.

Ningekuwa mjinga kumpuuza mkandarasi kwa sababu yoyote ile, iwe uchoyo, kiburi, au hata kuweka imani katika uzoefu wangu mwenyewe. Kufuata chochote isipokuwa mpango wa mkandarasi wa msingi imara ungesababisha maafa. Hivyo ndivyo hata kwetu kama waamini katika nyakati ambazo tunakosa kujua au tunapuuza maagizo ya Mungu. Haitoshi sisi kuwa "wasikilizaji," lakini lazima tuwe "watendaji" (Yakobo 1:22) ikiwa tunataka kujenga msingi imara wa maisha yetu. Daima ni upumbavu kwetu kuhoji au kumpuuza mbunifu wa imani yetu, Yesu Kristo.

Maandiko yanafunua habari juu ya uumbaji wa Mungu kwa kutumia msingi imara ambao nasi tunahitaji kujifunza na kufuata, kwa sababu jengo ni imara tu ikiwa msingi wake ni imara. Maisha yako yanaweza kuonekana mazuri kwa muda huku ukipuuza ukweli huu, lakini dhoruba zitakuja. Dhoruba za matatizo mwishoni zinafunua hali halisi ya msingi wako.

**Vipaumbele kwa kila Sehemu**

Yesu alituambia, "Bali utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33). Wakati wa kutafsiri "vitu hivi vyote" unahitaji kuzingatia kwamba mahubiri haya yanaanzia Mathayo 5:1, yajulikanayo kama Mahubiri ya Mlimani. Yanayohusiana na mazingira ya karibuni ni (mstari wa 31) yanazungumza juu ya chakula, vinywaji na mavazi. Ikiwa Kristo atashughulikia mahitaji yetu yote pindi tunapomtafuta yeye kwanza, je! Hatatupa vitu vingi zaidi katika ndoa zetu?

Kumtafuta Mungu na ufalme wake inatakiwa kuwa kipaumbele chetu kama waamini, kwa kuwa huo ndio msingi wa maisha. Kama waume na wake, ninyi pia ni wahudumu wa Mungu kwa wenzi wenu na mnatakiwa kuchukuliana na changamoto zinazotakana na ninyi kutimiza mapenzi yake katika mambo yote yanayohusiana na familia yenu. Tunatimiza haya kwa kuweka masuala ypte katika mtazamo wa kwamba, uchaguzi wetu uzingatie kile ambacho Mungu anasema ni muhimu. Ili tuweza kutimiza mapenzi yake, kwa hakika tunapaswa kumtazama yeye kila siku ili atuwezeshe kuwa na nguvu za kukamilisha kazi yake.

**FAILI LENYE UKWELI**
Tafuta kwanza- Amri ya kutenda Bila kuacha. Ahadi ni kwamba, kila unapotenda utazidishiwa.

Wengi wetu tutakubali kwamba ni muhimu kwa mchungaji kuwa na uhusiano imara, na wa karibu na Bwana. Tungetarajia angeamka kila siku na atumie muda wake kusoma na kuomba, akitafuta hekima na mwongozo kutoka kwa Mungu ili kuongoza familia yake na makutano. Ikiwa hakufanya hivyo, tungehoji kujitolea kwake tukitambua hitaji la uwezeshwaji wa Mungu kwake na mwongozo wa kutimiza majukumu yake.

Unaweza kuweka matarajio hayo haraka kwa mchungaji wako, lakini jifikirie mwenyewe. Kwa kuwa Mungu anaangalia kumtumikia mwenzi wako na watoto wako kwa umuhimu ule ule anaoweka juu ya uhusiano wa mchungaji na makutano yake, je! Sio jambo la haraka sana kwako pia kumtafuta Mungu kila siku? Je, sio lazima kwako kujenga msingi huo thabiti, yaani uhusiano huo na Kristo ambapo unapata nguvu na hekima inayohitajika kumtukuza Mungu katika familia yako? Uzoefu na Maandiko yanatuambia kwamba ikiwa hatusomi Neno na kuomba kila siku, asili ya dhambi ya zamani huanza kujitokeza, kuleta machafuko na uharibifu katika maisha yetu.

**Msingi dhaifu - Matatizo ya Familia**

Tunapoziangalia familia kote ulimwenguni, tunaona kuwa ziko matatizoni. Kiwango cha talaka ndani ya Kanisa kinaongezeka, wakati watoto wanauana, wanatumia dawa za kulevya na wanajihusisha na ngono. Wengi hata wanatembea mbali na imani. Kitabu kimoja kinasema hivi kuhusu watoto wa Marekani:

> Kati ya asilimia themanini na tisini ya watoto huko Marekani wanaacha imani za wazazi wao mara tu watakapokuwa watu wazima. Kwa kiwango hicho cha kusikitisha, watoto milioni hamsini ambao wako kanisani leo watatoweka na kufanya idadi kuwa hadi chini ya elfu saba katika vizazi kumi tu vijavyo. Hiyo ni ya kusikitisha ambapo familia za sasa za Kikristo huko Marekani zinaendelea bila kufanya mabadiliko yoyote makubwa. [9]

Washauri wa Kikristo wanaohudumia wanandoa na familia ambazo zinapitia majaribu makubwa, mara nyingi hugundua kwamba msingi wa imani imara na wa kudumu umepuuzwa. Mara nyingi, hii ni kwa sababu ya kukosa maarifa, ambapo watu hutenda kutokana na uzoefu na ushauri wa ulimwengu badala ya ukweli wa kibiblia. Kwa sababu wanandoa na wazazi hawajafundishwa jinsi ya kujenga msingi huu thabiti katika maisha yao wenyewe, ushawishi kama wa Kristo wanaopaswa kuwa nao kwa wenzi na watoto wao haupo tena. Kulea familia kwa njia yako na nguvu zako mwenyewe kunaweza kusababisha kumfanya mwenzi na watoto wako wamwache Mungu.

**Ukaribu na Mungu**

Katika Kumbukumbu la Torati 6, Musa alitimiza mapenzi ya Mungu kwa kuwafundisha Waisraeli kile kinachotarajiwa kutoka kwao pindi watakapoingia katika nchi ya ahadi. Ndani ya maagizo haya, Mungu hufunua moyo wake kuhusu uhusiano wa karibu anaotaka kuwa nao kwetu. Uhusiano huu wa karibu na Mungu ndio msingi, nguvu ya imani yetu, ambayo juu yake tunajenga maisha yetu na familia.

> Na hii ndiyo sheria na amri na hukumu, alizoziamuru Bwana, Mungu wenu, mfundishwe, mpate kuzitenda katika nchi ile mnayoivukia kuimiliki; upate kumcha Bwana, Mungu wako, kushika amri zake zote na sheria zake ninazokuamuru wewe na mwanao na mwana wa wanao, siku zote za maisha yako, tena siku zako ziongezwe. Sikiliza basi, Ee Israeli ukaangalie kuzitenda upate kufanikiwa, mpate kuongezeka sana, kama Bwana M ungu wa baba zako alivyokuahidia katika nchi ijaayo maziwa na asali.

> Sikiliza Ee Israeli, Bwana Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja, nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo yatakuwa moyoni mwako. (Kumbukumbu la Torati 6: 1-6)

Mstari wa 3 na wa 4 huanza na "Sikiliza, Ee Israeli" ili kusisitiza umuhimu wa kusikiliza sauti ya Mungu. Wakati wowote mistari hiyo inapoonekana, inamaanisha "Sikiliza!" Mungu yuko upande wetu kweli, na anataka tufanikiwe. Katika mistari hii, habari hiyo ilikuwa muhimu kwa Israeli kama taifa ili waweze kuishi. Kile ambacho Mungu alisema katika Kumbukumbu la Torati 6 ni muhimu kwetu leo. Mistari hii inafunua ukweli ambao pia ni msingi wa mafanikio yetu kama waamini na wahudumu kwa watoto wetu.

Mstari wa 5 unasema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote," inamaanisha unaonyesha upendo wako kwa Mungu kwa kuchagua kuwa na uhusiano naye wa karibu. Kutumia muda wako na Kristo ni jambo la kufanywa kila siku. Kufahamiana kwa karibu na kukaa ndani yake "kwa moyo wako wote, na roho yako yote, na nguvu zako zote" inaonyesha ushiriki wa ubinadamu wako kamili yaani; mwili, roho na nafsi. Unatambua kwamba mwenzi na watoto wako wanahitaji upendo kutoka kwako, hivyo unatakiwa kuwa na namna ya kulitimiza hilo.
Lakini Mungu pia muda binafsi pindi unapojenga uhusiano wa upendo pamoja naye. Mungu anaahidi kwamba ukimtanguliza yeye, mahusiano yako mengine yataboreshwa.

Mstari wa 6 unasema, maneno ya Mungu lazima yawe ndani ya mioyo yetu, ambayo inamaanisha kusoma Maandiko kila *wakati- na kuyatii*. Ili kumuiga Kristo na kuwafundisha wengine, lazima tuwe na ufahamu wa karibu wa mapenzi ya Mungu. Hivyo kutegemea hekima na nguvu za Kristo ndio msingi unaohitajika katika kutimiza majukumu magumu ya kuwahudumia wenzi wetu na kuwaongoza watoto wetu kwenye ukomavu wa kimungu. Matendo yetu ya kila siku ya kujitolea na mawasiliano ya karibu na Mungu yanahusiana moja kwa moja na mafanikio.

**FAILI LENYE UKWELI**

*Moyo-Lebab* (Kiebrania). Moyo, akili, mtu wa ndani. Matumizi ya kimsingi ya neno hili yanaelezea tabia nzima ya mtu wa ndani. [10]

*Moyo-Kardia* (Kigiriki). Kiti cha tamaa, hisia, mapenzi, tamaa, misukumo; moyo au akili. [11]

**CHIMBA ZAIDI**

Eleza tunapaswa kufanya nini na Neno la Mungu.

> Kwa moyo wangu wote nimekutafuta;
> Uniache nipotee mbali na maagizo yako!
> Nimeficha neno Moyoni mwangu nimeliweka neno lako,
> Nisije nikakutenda dhambi. (Zaburi 119: 10-11)

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Eleza ni jinsi gani kanuni hizi zinaweza kukusaidia kuwa mwenzi bora. Orodhesha njia mbili kwa kila mstari.

Lakini neno hilo li karibu nawe sana, li katika kinywani chako na moyo mwako, upate kulifanya.
(Kumbukumbu la Torati 30:14)

Sheria ya Mungu wake iko moyoni mwake;
Hatua zake hazitelezi. (Zaburi 37:31)

Kufanya mapenzi yako Ee Mungu wangu,
Ndiyo furaha yangu. (Zaburi 40: 8)

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

Cha kusikitisha ni kwamba, watu wengi walio katika Kristo hawajawahi kufundishwa ukweli kwamba urafiki na Mungu (Baba, Bwana Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu) uko sawa na kiwango cha bidii iliyowekwa katika kumtafuta yeye. Ukaribu huo unahitaji kuweka muda katika Neno lake, kuomba na kushirikiana na waamini wengine. Neno *lililofundishwa* linatuonyesha kwamba Mkristo mmoja (au kadhaa), pengine aliyekomaa zaidi katika imani, amekuja kusaidia mtu mwingine kukuza urafiki na Bwana; kwa maana bila mwongozo, njia inaweza kuwa ngumu kufuata.

Unaweza kuamini lakini pia ukajiuliza ni vipi inawezekana kukuza uhusiano na Mungu asiyeonekana. Unaweza kutathmini uhusiano wako na Mungu na kujiuliza ikiwa kuna kitu zaidi ya kwenda kanisani Jumapili, kuomba sala ya wokovu na kubadilisha tabia mbaya. Ndio, *kuna zaidi*, na unaweza kwenda zaidi katika uhusiano wako na Mungu.

## Somo la 7

## Vipengele vitatu Muhimu

Yesu alielezea umuhimu wa kuwa na msingi imara katika vipengele vitatu muhimu.

> Na kwa nini mnaniita "Bwana, Bwana," walakini hamyatendi nisemayo? Kila mtu ajaye kwangu, na kuyashika maneno yangu na kuyatenda, nitawaonyesha mfano wake: Mfano wake ni mtu anayejenga nyumba na kuchimba chini sana na kuweka msingi juu ya mwamba; na kulipokuja gharika, mto ulishukia nyumba ile kwa nguvu usiweze kuitikisa, kwa kuwa imejengwa vizuri. Lakini yule aliyesikia na hakutenda mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba juu ya ardhi pasipokuwa na msingi, mto ukaishukia kwa nguvu; ikaanguka mara. Na maangamizi yake nyumba ile yakawa mkubwa. (Luka 6: 46–49)

### Kumpokea Yesu Kristo

Kwanza, Alisema, "Yeyote ajaye kwangu," jambo ambalo linaonyesha mahali ambapo tunapaswa kujenga. Biblia iko wazi kuwa Yesu ndiye msingi wetu.

> Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka mtu mwingine isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani Yesu Kristo. (1 Wakorintho 3:11)

Lazima kuwe na nyakati maishani mwako ambapo unapaswa kutafuta msamaha wa dhambi zako na kumuomba Yesu Kristo aje maishani mwako kama Bwana na Mwokozi. Kuzaliwa tu Marekani na kuhudhuria kanisani hakukufanyi kuwa Mkristo. Wokovu unahitaji uamuzi wa kutubu dhambi na kugeuza mwenendo wa maisha yako kwa Mungu kupitia Yesu Kristo.

> Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndiyo wale wanaoamini jina lake. (Yohana 1:12)

### Uhusiano wa Kila Siku na Kristo

Pili, kifungu cha maneno katika kitabu cha Luka kinasema, "Yeyote. . . asikiaye maneno yangu,"ambapo humaanisha zana tunazotumia kujengea, ambazo ni Neno la Mungu na maombi. Lazima uamue kutumia muda wako mara kwa mara kusoma na kutafakari Neno la Mungu, ukisikiliza kwa dhati kabisa kile ambacho Mungu anasema. Kupitia Neno la Mungu na sala, tunamjua yeye na kuelewa upendo wake na jinsi ya kuishi kwa usahihi.

> Nimesulubiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai, wala si mimi tena bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili nanao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. (Wagalatia 2:20)

### Kutii Neno la Mungu

Tatu, lazima tuliishi au kutii Neno la Mungu. Wakati Yesu aliposema, "Yeyote. . . asikiaye maneno yangu na kuyashika", alikuwa akimwelezea mtu anayefanya mapenzi ya Mungu. Mchakato huu wa kusikia na kuyashika unamaanisha kutii, au kutumia Neno lake maishani.

> Na kwa nini mnaniita "Bwana, Bwana," walakini hamyatendi nisemayo? Kila mtu ajaye kwangu, na kuyashika maneno yangu na kuyatenda, nitawaonyesha mfano wake: Mfano wake ni mtu anayejenga nyumba na kuchimba chini sana na kuweka msingi juu ya mwamba; na kulipokuja gharika, mto ulishukia nyumba ile kwa nguvu usiweze kuitikisa, kwa kuwa imejengwa vizuri. Lakini yule aliyesikia na hakutenda mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba juu ya ardhi pasipokuwa na msingi, mto ukaishukia kwa nguvu; ikaanguka mara. Na maangamizi yake nyumba ile yakawa mkubwa. (Luka 6: 46–49)

> Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili, si kwa mbegu iharibikayo, bali ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele. (1 Petro 1: 22-23)

Andika vipengele hivyo vitatu kwa maneno yako mwenyewe.

1. ______________________________________________
2. ______________________________________________
3. ______________________________________________

Maandiko yanatuambia kuwa ni muhimu kuendelea kuchunguza nia na matendo yetu.

> Na tuchunguze njia zetu na kuzijaribu,
> Na mrudi Bwana tena. (Maombolezo 3:40)

**Kujichunguza**

Eleza jinsi unavyoendesha uhusiano wako wa kila siku na Mungu katika maeneo ya sala na kusoma Neno lake na kulitumia. Unawezaje kuelezea ubora wa msingi wako wa kiroho?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

***MPANGO KAZI 1***

Baada ya kujifunza kanuni hizi, je! Kukiri na kuomba msamaha kunahitajika? Andika sala yako na kujitolea kuanza kila siku pamoja naye.

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

______________________________________________________________________________
__________________________________________________

**Yesu kama Msingi**

Na tuchunguze vipengele vitatu ambavyo Yesu alisisitiza katika Luka 6: 46-49.

Je! Umekubaliana na Mungu kuhusiana na injili, kwamba wewe ni mwenye dhambi na kwamba Kristo alikufa msalabani kama malipo ya dhambi hizo, na kwamba alizikwa na kufufuka siku ya tatu (1 Wakorintho 15: 3-4)? ___ Ndio/Hapana

Je! Umemuomba Mungu akusamehe dhambi zako na kumwalika Yesu moyoni mwako, kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yako? ___ Ndio/Hapana

Hii ni hatua ya kwanza muhimu ya kujenga msingi imara. Huwezi kuruka hii, kwa sababu Kristo ndiye msingi wa imani yetu. Ikiwa bado hauna uhakika, kagua *Kiambatisho B: Kujitolea Maisha Yako kwa Kristo* kwa maelezo zaidi.

> Kwa sababu umkikiri Yesu kwa kinywa chako kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika kwa wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. (Warumi 10: 9-10)

Unaweza kuomba sasa kumwalika moyoni mwako na sala rahisi kama hii:

> *Bwana Yesu, nakiri kwamba mimi ni mwenye dhambi, na ninakuja kwako kusamehewa. Ninaamini Ulilipia dhambi yangu kwa kufa msalabani, na ninaamini ulizikwa na kufufuka kutoka kwa wafu siku ya tatu. Asante kwa dhabihu yako. Tafadhali ingia moyoni mwangu, unijaze na Roho wako Mtakatifu, na unisaidie kuwa mwanafunzi wako. Asante kwa kunisamehe na kuja katika maisha yangu. Asante kwamba sasa mimi ni mtoto wa Mungu na kwamba ninaenda mbinguni. Amina.*

**Umuhimu wa Maombi**

Baada ya kuchagua kujenga maisha yako juu ya imani ya Yesu Kristo, vipengele viwili vifuatavyo vinahusu kumfuata Kristo kwa kuweka vipaumbele. Wacha tufikirie mafanya maombi. Maombi huaminiwa kama jaribio la kuomba nguvu za Mungu katika kubadilisha hali, lakini Mungu anavutiwa zaidi na kuwa na ushirika wa kifikra na sisi mara kwa mara.

Maombi ni kazi ya mawazo, lakini zaidi ya hayo, ni njia ya wazi ya mawasiliano na Mungu ambayo inajumuisha kuongea na kusikiliza. Mungu anataka ujue kuwa yeye yupo kwa ajili ya vitu vyote wakati wote.

> Msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno, kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zetu na zijulikane na Mungu. (Wafilipi 4: 6)

Mungu anatamani tuwe na ufahamu wa kudumu kuhusu uwepo wake, pawe na mawasiliano endelevu na pia anataka utumie muda wa utulivu, wa faragha pamoja naye kila siku. Katika Zaburi 5: 3, Daudi alisema, "Utasikia sauti yangu asubuhi, Ee Bwana; asubuhi nitaielekeza kwako, nami nitaangalia juu."

Maombi na kusoma Biblia ni vitu muhimu kwa ukuaji katika maisha ya Kikristo. Wakati huu wa kusoma na mawasiliano mara nyingi huitwa ibada. Kujihusisha naye kwelikweli ni zaidi ya neno lenyewe lililoandikwa, kwani inahitaji hali ya mawazo inayoitwa imani - kuamini ingawa hatuwezi kuona. Katika Yohana 20:29, Yesu alisema, "Kwa sababu umeniona, umeamini. Heri wale ambao hawajaona lakini wameamini. "

Katika Mathayo 6: 9-13, inayoitwa Sala ya Bwana, Yesu mwenyewe alitupa mfano wa jinsi alivyoomba na kufunua mambo kadhaa ya msingi ya kuzingatiwa katika maombi.

Sala ifuatayo ni mfano wa kukusaidia kuelewa unyenyekevu wa mawasiliano ya kutoka moyoni yaliyoongozwa na mambo muhimu katika sala ya Bwana na inaweza kutumika kuanza muda wako wa ibada.

*Bwana Yesu, nakushukuru na kukusifu kwa kutamani kuwa karibu nami, kwa kutaka kutumia muda na mimi. Ninakushukuru kwa upendo wako na uaminifu wako, na ninakusifu wewe, Mungu muumba na mtunzaji wa vitu vyote. Ninaomba neema ya kutembea kwa utii leo, kumpenda mwenzi wangu na watoto wangu, na kuwajali kulingana na Neno lako. Nisaidie kumsamehe mtu yeyote ambaye ananiumiza leo, na nipe neema ya kuomba msamaha wakati ambao nitashindwa kukuwakilisha. Na, Yesu, tafadhali fungua moyo wangu kupokea Neno lako asubuhi ya leo. Ninaomba ufahamu, kukujua zaidi, na neema ya kua mtiifu. Amina.*

Ni muhimu kuanza muda wako wa ibada kwa maombi, au pengine kitu sawa na hiki. Unaweza kushawishiwa kutumia maombi yaliyoandaliwa, lakini shauku kubwa ya Mungu ni kuzungumza na wewe tu. Baada ya yote, yeye tayari anajua kilicho moyoni mwako na anakupenda licha ya kile ulichofanya. Warumi 5: 8 inasema, "Mungu anaonyesha upendo wake mwenyewe kwetu, kwa kuwa wakati tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu." Unapotumia muda kila siku na Mungu, utaanza kujisikia raha katika upendo wake, na kuomba itakuwa "kuzungumza naye" juu ya kila kitu.

***MPANGO KAZI 2***

Andika sala kwa Mungu, ukiomba msaada katika kukuza maisha ya ukaribu naye pamoja na maombi. Kumbuka kwamba ni kwa imani tu katika Kristo ndio tumepewa njia ya kumfikia Baba. Katika Yohana 14: 6, Yesu alisema, “Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima. Hakuna anayekuja kwa Baba ila kwa njia yangu. ”

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

Soma sala hii ambayo Paulo alitoa kwa Waefeso. Matamshi huweza kubadilishwa kuifanya iwe ya kibinafsi kwako.
Fanya iwe ya kibinafsi zaidi kwa kuweka jina lako mahali ambapo mstari tupu unaonekana.

> Kwa sababu hii mimi [_________________] ninapiga magoti kwa Baba wa Bwana wetu Yesu

> Kristo, ambaye kutoka kwake familia zote mbinguni na duniani zimepewa jina, kwamba anipe [kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kutiwa nguvu ndani yangu kupitia Roho wake Mtakatifu, ili Kristo akae ndani yangu [moyoni wangu] kupitia imani; ili [mimi], nikiwa nimekita mizizi katika msingi wa upendo, niweze kuuungana na watakatifu wote katika kujua kwa upana na urefu na kina - kujua upendo wa Kristo ambao hupita maarifa; ili [nijazwe] utimilifu wote wa Mungu.
>
> Kwa hiyo nampigia baba magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa duniani na mbinguni unaitwa, awajalie kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake… Amina. (Waefeso 3: 14-21)

Orodhesha maombi maalum au sifa ambao Paul alizijumuishwa katika sala yake.

______________________________________________________________________________
________________________________________________

______________________________________________________________________________
________________________________________________

______________________________________________________________________________
________________________________________________

______________________________________________________________________________
________________________________________________

______________________________________________________________________________
________________________________________________

Pamoja na kuifanya sala hii kuwa ya binafsi, unaweza pia kuitumia mara kwa mara kuomba vitu hivi katika maisha ya mwenzi wako na watoto wako, na wapendwa wengine, kwa kuingiza majina yao.

Mungu anatamani uhusiano, ambao unahitaji kuamini injili na kujitolea maisha yako kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi na uchague kutenga wakati wa kuomba na kusoma Neno lake.

Kuishi maisha ya Kikristo, wakati mwingine hujulikana kama "kukaa ndani ya Kristo," inajumuisha kumsikiliza Mungu kwa kusoma na kutafakari Neno lake. Katika Mathayo 4: 4, Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate peke yake, bali kwa kila neno litokalo kinywani mwa Mungu." Mchungaji wako anaweza kuwa mwalimu wa ajabu, lakini kuishi kwa wiki zima kwa kutumia ujumbe wa Jumapili peke yake kutasababisha kuwa dhaifu kiroho.

Wakristo wengi hutunza vijitabu vya ibada, kwa mfano kitabu cha *mkate wetu wa kila siku*, bafuni au kando ya kitanda wakiamini wanaweza kupata haraka nguvu ya kiroho. Wanaweza kuvigusa na kusoma kidogo kisha wanafikiri kufanya mambo yao mengine. Lakini, chakula cha haraka kama hiki huisha karibu, ni kama kumbukumbu ya kile tunachosoma haraka hupotea haraka. Katika tamaduni zetu tuna vifaa vingi vya kutusaidia kufanya kazi nyingi kwa mara moja na pengine wakati wetu na Mungu huwa sehemu ya mchanganyiko wa mambo ya kila siku. Ikiwa hatuweki bidii kwa kutenga wakati wa kila siku peke yetu na Mungu, pamoja na kusoma kwa umakini, kutafakari na sala, basi tunaweza kuanguka katika uharibifu wa ghafra, ambao bila shaka utasababisha afya mbaya ya kiroho.

**CHIMA ZAIDI**

Jifunze mistari ifuatayo na andika wanachosema juu ya mtazamo ambao tunapaswa kuwa nao wakati wa kusoma Neno na kutafuta hekima kutoka kwa Mungu.

> Moyo wa mwenye busara hupata maarifa,
> Na sikio la wenye hekima hutafuta maarifa. (Mithali 18:15)

________________________________________

________________________________________

________________________________________

> Inunua ukweli, wala usiiuze,
> Naam, mafundisho na ufahamu. (Mithali 23:23)

________________________________________

________________________________________

________________________________________

> Mwenende kama ulivyo wajibu kwenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa,
> mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu.
> (Wakolosai 1:10)

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Ili kuepuka kusoma kwa haraka, jenga tabia ya kutafakari Neno la Mungu. Watu wengi hufikiria sala za Wahindu wanaposikia neno *kutafakari*, lakini ni neno linalotumiwa na Mungu wa Biblia. Kutafakari ni njia ya kuzungumza na Mungu bila maneno. Tunapoacha kutafakari juu ya kile tunachosoma, tunakua na ustadi wa kusikiliza tu bila kuweka katika mawazo yetu kile ambacho Mungu anasema. Biblia inasema "tulia" mbele za Mungu ili aweze kuwasiliana nasi.

> Nitayatafakari mausia yako,
> Nani nitaziangalia njia zako. (Zaburi 119: 15)

**FAILI LENYE UKWELI**

*Tafakari* -Katika ulimwengu wa kibiblia, kutafakari haikuwa mazoea ya kimya. Ilimaanisha kulia, kutamka, au sauti za kunung'unika, kama kusoma nusu kwa sauti au kuzungumza na wewe mwenyewe, kuingiliana na maandishi ili iweze kuingia kwenye akili yako. Kama vile begi la chai linaloingia ndani ya maji linavyopenya majimaji, vivyo hivyo kutafakari juu ya Maandiko kunaingia katika akili zetu.

**CHIMA ZAIDI**

Tambua kile ambacho Mungu alimwambia Yoshua afanye na kwanini ilikuwa muhimu sana kwa Mungu na kwa mafanikio ya Yoshua.

> Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na yote yaliyoandikwa humo. Maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapofanikiwa sawa.
> (Yoshua 1: 8)

______________________________________________________________________________
_____________________________________

______________________________________________________________________________
_____________________________________

______________________________________________________________________________
_____________________________________

Je! Unataka kuwa na "mafanikio mema" katika ndoa yako? ___ Ndio/hapana

Eleza maana ya kifungu hiki kwako. Je! Kulichukua hili kwa moyo na kuishi kuliishi kutaathiri ndoa yako?

> Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki,
> Wala hasimami katika njia ya wakosaji,
> Wala hahuketi barazani pa wenye mizaha;
> Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo,
> Na sheria yake hutafakari mchana na usiku.
> Naye atakuwa kama mti iliyopandwa kandokando ya vijito vya maji,
> Huzaao matunda yake kwa majira yake.
> Wala jani lakehalinyauki;
> Na kila afanyalo litafanikiwa. (Zaburi 1: 1-3)

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________

## Somo la 8

## Mungu Anahitaji Upendo Wako

Kipindi watoto wanapokuwa wadogo, huku wakiwategemeza mama na baba kwenye kuwahudumia inaweza kuwafanya kounekana wasumbufu au waoga wakati wanapoachwa katika uangalizi wa mtu mwingine. Wakati mama au baba wanaporudi, kuna mapenzi na furaha kubwa huonekana kwao. Kila wakati uhusiano mzuri wa mzazi na mtoto hutoa huzaa upendo mkubwa kati yao. Watoto wanakuwa wakubwa, wanakuwa huru zaidi na uhitaji mkubwa juu ya kuungana huku unafifia. Labda salamu ya kawaida kama "Hujambo Mama" au "Salama Baba’’ bado hazitoshi kwao. Katika muungano huo, uwepo wa wazazi huchukuliwa kama jambo la kawaida tu na pengine na hautambuliki kabisa.

Tunaweza kufanya jambo hilo hilo kwa Bwana. Tunapokuja kwa Kristo kwa mara ya kwanza, hatuwezi kungojea kuomba tu na kisha kuingia kwenye Neno, kwa kulisoma, ndipo tunahisi Mungu akizungumza na mioyo yetu. Mara kwa mara hali hii hutupa hisia nzuri na hata kutufanya kushirikisha habari zetu njema na marafiki na wapendwa. Jihadharini na kuanguka katika hali ambapo Neno la Mungu linakuwa la pili katika akili zetu ukilinganisha mapendeleo yetu mengine; wakaki ambao mambo mengine ya maisha yanakuwa muhimu zaidi kuliko wakati wetu na Mungu.

Tusipo kuwa makini, mitazamo yetu inaweza kuwa “Ndio, ndio, kusoma Mathayo tena. Najua, nilishasoma nikamiliza.” Kwa kusikitisha, tunapoteza mtazamo wa "Baba yuko hapa!" Hatuwezi kukaa katika hali hii, Tuna bahati iliyobarikiwa ya kuingia Patakatifu pa Patakatifu na Mungu anayetaka tumwite "Baba" kama Warumi 8:15 inavyosema, "Abba, Baba." Tumsikie akinong'ona ukweli wa kushangaza na kutuambia jinsi tulivyo wa ajabu na muhimu kwake.

**Kujichunguza 1**

Ni lini mara ya mwisho ulikaa kimya na Mungu aliye hai, ukisubiri kwa hamu azungumze nawe?

______________________________________________________________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________________________________________________________________

Baada ya Yesu kutoa roho yake pale msalabani, tukio la kwanza lililorekodiwa katika Biblia lilikuwa ni kupasuka kwa pazia, kutoka juu hadi chini, ambalo lilifunikwa mlango wa chumba cha hekalu kiitwacho Patakatifu pa Patakatifu (Mathayo 27:51). Ilimaanisha kwamba kifo cha dhabihu cha Kristo kilimaliza kutengana kwetu na Mungu. Kabla ya hapo, ni kuhani mkuu tu ndiye angeweza kuingia hapo mara moja kwa mwaka akibeba damu ya mnyama wa kafara. Gharama kubwa ililipwa wakati Kristo alipojitolea damu yake mwenyewe kwa ukombozi wetu. Waebrania 10:19 inasema, "Kwa hiyo, ndugu, tukiwa na ujasiri wa kuingia Patakatifu pa Patakatifu kwa damu ya Yesu," inatuhakikishia kwamba kifo cha Yesu haikuwa tu kushinda nguvu ya dhambi bali ni kununua njia ili Baba awe na ushirika wa karibu na sisi. Hatupaswi "kupuuza wokovu huo mkuu" (Waebrania 2: 3).

Ikiwa una watoto wakubwa, umebarikiwa kiasi gani pindi wanapotaka kutumia muda na wewe? Je! Unafikiri Mungu ni tofauti? Anafurahia pindi tunapotenga muda na kusema kusema, "Baba, huu ni wakati wako, muda wangu na wako tu kwa sasa na sitakubali kitu chochote kikwamishe. Nitailinda hii, Mungu."

Pindi tunapoweka ahadi hii ya kutenga wakati kwa ajili ya Mungu, usumbufu unaonekana kutoka katika kazi zetu ngumu, kama sio kutoka kwenye familia na simu zetu, basi akili hujaa mawazo kama vile; matatizo ya kazini, bili, mwenzi wako, watoto wako, n.k. Mara nyingi Shetani hutuma usumbufu huo kwa sababu anajua msingi wetu imara na nguvu ya imani yetu havitokani na sisi wenyewe, au tamaa yetu ya kuwa baba, mama, au mwenzi bora, bali vyote hutokana na uhusiano wetu na Kristo. Kila kitu kizuri kinafanikiwa kutokana na uhusiano huu.

**CHIMA ZAIDI**

Eleza ni nini mistari hii inasema juu ya vita tuliyomo na kile tunachopaswa kufanya.

> Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili.
> maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo/nguvu katika Mungu
> hata kuangusha ngome,tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka,
> kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara nyara kila fikira ipate
> kumtii Kristo. (2 Wakorintho 10: 3-5)

__________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

Wakati Yesu alipoelezea mfano wa mpanzi kwa wanafunzi wake (Marko 4: 13-20), alitaka wajue kuhusu mkakati wa Shetani. Je! Maandiko haya yangehusiana vipi na wakati wako katika Neno? Vita ni nini?

> Hawa ndio wale walio kando ya njia lipandwapo neno, na wakiisha kusikia,
> mara huja Shetani akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao. (Marko
> 4:15)

__________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

__________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________________

Wakati Paulo alipoandika 2 Wakorintho 11:3, alirejelea Mwanzo 3, ambayo inaelezea jinsi dhambi ilivyoingia ulimwenguni wakati Hawa alipokubaliana na uwongo wa Shetani. Hofu ya Paulo ni kwamba Shetani, vile vile, angeharibu (na kuharibu tena) akili za waamini wapya wakatoka kwenye unyenyekevu (usafi wa moyo) [12] ambao walikuwa nao katika uhusiano wao na Kristo.

> Lakini nachelea kama vile yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila zake, asije akaziharibu fikra zenu mkauach ausafi na unyofu kwa Kristo. (2 Wakorintho 11:3)

Hawa alidanganywa (kuongozwa na makosa) na ujanja wa Shetani (ujanja ujanja) ili aamini uwongo kuwa ukweli. Mpango wa Shetani ni ule ule kila wakati.

**Kujichunguza 2**

Je! Ni uongo gani umeamini juu ya shauku ya Mungu ya kuwa na uhusiano wa karibu na wewe?

Orodhesha mawazo ya kawaida ambayo huja wakati wa kuanza au kufanya ibada yako, na omba msaada wa Mungu kuyapinga.

Shetani hawezi kulaumiwa kwa kila kitu, wakati mwingine sisi wenyewe tunakosea. Wakati Yesu alipokuwa akisali katika bustani, huku akiugua kwa sababu alikabiliwa na kwenda msalabani, wanafunzi wake walilala wakati walipaswa kusali pamoja naye. Yesu aliwaonya juu ya udhaifu wa mwili.

> Keshani muombe msije mkaingia majaribuni. Roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu. (Mathayo 26:41)

Amri ya Yesu ni "kukesha na kuomba," na matokeo yake ni kwa faida kwetu - kwamba tusizidiwe na majaribu na uvivu wetu. Kuomba ni nidhamu muhimu ya kupigana vita dhidi ya mawazo kama vile *sijisikii kufanya hivyo*, *nimechoka*, *sijali*, au *sina muda*. Vipaumbele katika kumtafuta Bwana lazima vichukuliwe kwa uzito siyo kuwa kama mjadala wa ziada.

**CHIMBA ZAIDI**

Eleza ni nini mistari hii inakuelekeza ufanye.

> Mwe na kiasi na kukesha, kwa kuwa mshitaki wenu ibilisi, kama simba angurumaye huzunguka zunguka, akitafuta mtu ammeze.(1 Petro 5: 8)

> Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuzipinga hila za shetani. (Waefeso 6:11)

Mafanikio yako yote, pamoja na nguvu ya kuhudumu kama mume au mke, vinatokana na uhusiano endelevu na Kristo. Marko 4:34 inasema, "Na walipokuwa peke yao, aliwaelezea wanafunzi wake mambo yote." Kutumia wakati na Yesu katika ibada za kila siku na sala kutatupa ufahamu mkubwa katika Maandiko na pia nguvu na hekima tunayohitaji kwa ajili ya ndoa zetu.

Mungu anapenda kila mmoja wetu kwa usawa na anatamani kuzungumza nasi. Hakuna kitabu cha ndoa kilichoandikwa ambacho kitashughulikia kila hali unayokabiliana nayo. Hitaji letu kubwa sio suluhisho tu la shida zetu lakini mabadiliko ya ndani ya moyo ambayo ni Mungu tu anayeweza kuyatimiza kwa ajili yetu. Ndio sababu anataka sisi tumtegemee yeye kila siku, tukitafuta Neno lake kwa ajili ya ufahamu na mwongozo.

**CHIMA ZAIDI**

Tazama mawazo ya wanafunzi wakati ambao hawakuwa wameyaelewa mafundisho ya Yesu. Walifanya nini?

> Kisha Yesu akawaaga makutano akaingia nyumbani. Wanafunzi wake wakamwendea, wakamwambia, "Tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni." (Mathayo 13.36)

Mungu daima anatungojea tumwendee, akitaka tutafute hekima tunayohitaji kukabiliana na maisha yetu. Kwa kulijua hili, tunawezaje kuwa na shughuli nyingi kuliko wakati na Mungu aliye hai? Tunahitaji kuweka hii akilini kila wakati, tujilinde dhidi ya mwelekeo wetu wa kujitegemea au kuuchukulia wema wa Mungu kwa wepesi.

> Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtendakazi asiye na sababu ya kutahayari akitumia kwa hiyari Neno la ukweli. (2 Timotheo 2:15)

Mungu anasisitiza umuhimu wa kuwa na bidii katika kutumia wakati kwenye Neno lake ili tuweze kulifahamu kabisa au kuja kwenye tafsiri sahihi ya Neno.

**FAILI LENYE UKWELI**

*Jifunze* (kitenzi cha amri) - Agizo la kufanya na kuendelea kufanya. Kuendelea kwa bidii, kuwa na bidii, kufanya kila juhudi kufanya bora zaidi, kuwa na hamu na bidii katika kutimiza lengo.

*Suala zuri kugawa* -wazo la kukata kitu sawa kama wewe ungekuwa katika useremala au uashi, au na kukata kitambaa kuwa kushonwa pamoja.

Je! Unaweza kujipa daraja gani katika wakati wako wa ibada ya kila siku? ______

Je! Unafikiri Mungu anamaanisha nini hapa katika neno *asiye na sababu*?

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

***MPANGO KAZI 1***

Tafakari juu ya mstari huo kutoka kwa Timotheo. Andika sala kwa Bwana, ukiomba msaada maalum kufuata maagizo yake.

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

Tambua maonyo katika mstari huu.

> Kwa hiyo, ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu, maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. (2 Petro 1:10)

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

_______________________________________________________________________________
__________________________________________________

**Utii ni Hatua**

Kitu cha tatu kinachohitajika ili kujenga msingi imara wa maisha ni utii, au uamuzi wa kutenda kulingana na ukweli wa Mungu na mapenzi yaliyofunuliwa.

> Kila mtu ajaye kwangu na kuyashika maneno yangu, nitawaonyesha mfano wake. Mfano wake ni kama mtu ajengaye nyumba na kuchimba chini sana na kuweka msingi juu ya mwamba; na kulipokuja gharika mto ukiishukia nyumba ile kwa nguvu usiweze kuitikisa, kwa kuwa imejengwa vizuri. (Luka 6: 47-48)

Tunahitaji kuichukulia Biblia kama maneno ya Mungu. Katika nyakati za Agano la Kale, Wayahudi waliliona jina la Mungu kuwa takatifu sana hivi kwamba hawakuthubutu kulitaja. Tunahitaji kutambua jinsi tulivyomebarikiwa sana kwa sasa kwamba neema ya Mungu, iliyoonyeshwa na dhabihu ya Yesu msalabani, imetutangaza kuwa hatuna hatia na imetuwezesha kumfikia Baba mbinguni na uwepo wa Roho Mtakatifu kama mwalimu na kiongozi. Sehemu yako ni kutamani kufanya mapenzi yake na kujibu kwa shukrani na utii. Ikiwa unalichukulia Neno la Mungu kama chaguo la ziada, basi unaweza kujikuta ukichagua na kuchukua kile kinachofaa mapenzi yako binafsi. Hiyo itasababisha uwe na msingi dhaifu wa maisha yako.

> Basi kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha
> vyote alivyonavyo si mwanafunzi Wangu. (Luka
> 14:33)

> Kwa ajili ya hayo wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena.wala hawakutembea naye tena. Basi Yesu akawaambia wale thanashara, "Je, ninyi nanyi mwataka kuondoka?" (Yohana 6: 66-67)

***MPANGO KAZI 2***

Andika nia ya kujitolea kwa Mungu, katika kumtegemea yeye kwa neema na nguvu zake, kwenu nyote kama mume na mke, kutamani na kufuata maagizo yake.

______________________________________________________________________________
____________________________________________________

______________________________________________________________________________
____________________________________________________

______________________________________________________________________________
____________________________________________________

______________________________________________________________________________
____________________________________________________

Mungu aliweka moyo wake katika vipaumbele vyetu, kwamba baada ya Mungu, familia yako lazima iwe kipaumbele katika mawazo yako, mapenzi, na matendo, hii inahusiana na kuihudumu ipasavyo. Familia nyingi ziko nje ya utaratibu, watu wanajali zaidi juu ya burudani, kazi, au hata huduma kanisani.

> Huu ni ni usemi wa kiimani: Ikiwa mtu anatamani nafasi ya Askofu, anatamani kazi nzuri. Basi Askofu hana budi kuwa mtu asiye na lawama, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi, mwenye tabia njema, mkaribishaji wageni, anayeweza kufundisha; si mlevi, si mkali, si mlafi wa pesa, bali ni mpole, si mgomvi, si mwenye tamaa; anayetawala vizuri nyumba yake mwenyewe, akiwa na watoto wake kwa kutii kwa heshima zote (kwa maana ikiwa mtu hajui kutawala nyumba yake mwenyewe, atalishughulikia vipi kanisa la Mungu?), si mwanzilishi, asije akajivuna kwa kiburi akaanguka katika hukumu ile ile kama ibilisi. Isitoshe lazima awe na ushuhuda mzuri kati ya wale walio nje, asije akaanguka katika laana na mtego wa Ibilisi.
>
> Vivyo hivyo, mashemasi wanapaswa kuwa wacha Mungu, wasiwe na lugha mbili, wasiwe wenye kunywa divai nyingi, wasiwe na tamaa ya pesa, wakishika siri ya imani kwa dhamiri safi. Lakini na hawa pia wajaribiwe kwanza; basi na watumike kama mashemasi, wakionekana kuwa hawana lawama. Vivyo hivyo, wake zao wanapaswa kuwa wacha Mungu, sio wachongezi, wenye kiasi, waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakitawala watoto wao na nyumba zao vizuri. Kwa wale ambao wamehudumu vizuri kama mashemasi wanapata wenyewe msimamo mzuri na ujasiri mkubwa katika imani iliyo katika Kristo Yesu. (1 Timotheo 3: 1-13)

Kuhusu mistari hii mwandishi mmoja alisema, "Paulo alionyesha kuwa uzoefu ambao kiongozi anaupata nyumbani unajenga upendo mkubwa kwenye jukumu lake kanisani." Kitenzi *kusimamia* kilionekana katika mstari wa 4. Kukuzwa kwa stadi sahihi za uongozi nyumbani ilikuwa sharti la kutumika kanisani. [13]

**Kujichunguza 3**

Mchungaji lazima awe na familia yake vizuri kabla ya kufuzu machoni pa Mungu ili aweze kuwa mfano bora kwa waamini. Ikiwa ungekutana na mchungaji aliye na shida dhahiri ya ndoa na familia na ukaona kwamba hakuwa akimwangalia mkewe au watoto kwa usahihi, je! Ungemheshimu yeye na uongozi wake? Kwa nini?

> Kwa maana nimemjua ya kwamba awaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake, waishike njia ya Bwana, kutenda haki na hukumu, ili Bwana naye akamtimizie Ibrahimu ahadi zake. (Mwanzo 18:19)

Huo ni mfano bora wa mtazamo wa Mungu kuhusu familia. Mungu alimwambia Ibrahimu, mume na baba, kwamba alimfahamu kwa kusudi, kuifundisha familia yake katika njia za Bwana. Tazama kwamba Mungu hakusema, "Unahitaji kufanya kazi kila wakati kuleta pesa taslimu," ingawa tunajua ikiwa hatutoshelezi familia yetu, tumekataa imani (1 Timotheo 5: 8). Yeye hasemi, "Fanya huduma zaidi" au "Kwanini usipandishe ngamia huyo na kuelekea chini kwenda Misri kupumzika." Ingawa kazi, huduma, na wakati wa kupumzika ni muhimu na hata ni ya kibiblia, lakini si kipaumbele cha kwanza. Usawa lazima uwepo, lakini kipaumbele chako cha kwanza ni uhusiano wako na Mungu, kisha familia.

**Kujichunguza 4**

Fikiria vipaumbele vyako kuhusiana na Mungu, mwenzi, watoto, kazi, Kanisa, burudani, na ushirika. Je! Mungu amekuwa wa kwanza, kisha familia? Muulize mwenzi wako ikiwa wanakubaliana na tathmini yako. Ikiwa una watoto, waulize kwa upole, kwa njia unayoweza kufundishika, na watakupa jibu moja kwa moja. Ikiwa vipaumbele vyako haviko sawa, andika sala ya kujitolea kubadilisha, kuwa mahsusi.

**CHIMA ZAIDI**

Eleza kile ambacho Maandiko haya yanasema juu ya dhana za kibiblia za kuchagua, kutumikia, na familia.

> Nanyi kama mtaona ni vibaya kwenu kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakayemtumikia, kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu wakiitumikia ng'ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori, ambao mnakaa katika nchi yao. Kaa; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana. (Yoshua 24:15)

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

> Naye Eliya akawakaribia watu wote, akanena, "Mtasitasita katikakti ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuate; bali ikiwa Baali, ni Mungu mfuateni yeye. Wale watu hawakujibu lolote. " (1 Wafalme 18:21)

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

> Hakuna mtu awezake kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyo, au atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Huwezi kumtumikia Mungu na mali. (Mathayo 6:24)

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

___________________________________________________________________________
__________________________________________________

Je! Unatumia kanuni za kimungu katika nyumba yako? Matunda ya Roho Mtakatifu ni "upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, uaminifu, upole, na kujidhibiti" (Wagalatia 5: 22-23). Je! Hizi ndizo sifa ambazo mwenzi wako na watoto wako wanaona zikikua ndani yako na zinaongezeka katika mazingira ya nyumbani kwako?

Je! Utajitathmini namna gani? ___ Kiasi kikubwa ___ Hujaribu na kuacha ___ Bado una sehemu nyingi za kukua

Ikiwa kitu kingine chochote kitakuwa muhimu zaidi kuliko uhusiano wako na Kristo, utateseka na familia yako pia. Mungu hubariki utii. Kutotii hukatisha baraka za Mungu kwa sababu tunafanya kazi katika mwili, kwa uasi na tuko nje ya mapenzi ya Mungu.

Je! Unaona maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa? Mungu hutupa maagizo, huyaweka wazi zaidi yaweze kueleweka, na anahitaji utii. Tunaye Roho Mtakatifu katika kulifanya Neno liwe hai ndani mwetu, kutufundisha, kutuongoza na kutuhakikishia tunapokuwa nje ya mapenzi ya Mungu. Sisi sote tunahitaji nguvu na neema ya Mungu kila siku. Lakini hatupaswi kusahau kamwe kwamba Mungu hafanyi hivyo kwa miujiza anatutaka tufanye kwa utii.

Kwa mara nyingine tena, orodhesha vipengele vitatu muhimu kwa ajili ya msingi imara.

1. ______________________________________________
______________________
2. ______________________________________________
3. ______________________________________________

## Somo la 9

## Jiwe Kuu la Pembeni

Kipengele muhimu zaidi cha kujenga juu ya msingi imara ni uteuzi wa jiwe kuu la pembeni. Ngoja tutazame kile ambacho Maandiko yanasema juu ya hilo kwa uhusiano na Kristo na pia uhusiano wetu na yeye.

> Basi tangu sasa, ninyi si wageni wala wapitaji; bali ninyi wenyeji pamoja na watakatifu; watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. (Waefeso 2: 19-20)

> Kwa kuwa imeandikwa katika Maandiko, "Tazama, naweka Sayuni
> Jiwe kuu la pembeni, mteule, teule lenye heshima,
> Na kila amwaminiye hatatahayari”
> Basi heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini
> Bali kwao wasioamini,
> "Jiwe walilokataa waashi limekuwa jiwe kuu
> la pembeni."
> Tena
> "Jiwe la kujikwaza mguu na mwamba wa kuangusha
> Kwa maana hujikwaza kwa neno lile wasiliamini,
> nao waliwekwa kusudi wapate hayo." (1 Petro 2: 6-8)

Kuna mpangilio wa maendeleo ya kiroho yaliyowasilishwa katika mistari hiyo:

1. Mpokee Yesu Kristo,
2. Kaeni ndani yake, na
3. Kutii.

Wakristo wengi hujishughulisha na hatua ya tatu. *Lo, sina budi kuacha kufanya hivi. Lazima nifanye kitu bora. Maisha yangu hayatampendeza Mungu kamwe.* Kwa bahati nzuri, kukamilisha hatua mbili za kwanza huleta mafanikio kwa hatua ya tatu - tunajikuta na nguvu, neema, na shauku ya kuwa waamini na watiifu.

Kipindi watu wanapokuja kwa ajili ya ushauri wakipambana na tabia mbaya au uraibu, swali la kwanza linapaswa kuwa, "Je! Uhusiano wako wa karibu na Kristo ukoje?" Jibu la kawaida ni, "Hiyo inamaanisha nini?" Uhusiano wetu na Kristo ni uhusiano ambao unatupa nguvu ya kutii. Urafiki wetu na Mungu ndio unatupa neema kwa siku ya kupata ushindi juu ya dhambi. Yeye *tu* anatupa neema kwa siku, hatupi neema kwa wiki moja hivyo tunahitaji kuona uhusiano huu na kuelewa kanuni hii ya kiroho. Mungu aliiunda kanuni hii kwa njia hii ili tuweze kudumisha ushirika wa kila siku na urafiki naye.

> Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuza peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu, kadharika na nyinyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi. Yeye akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huzaa sana; kwa maana bila mimi hamwezi kufanya neno lolote. (Yohana 15: 4-5)

Yesu amejikita katika wazo la kukaa, akitumia neno hilo mara nne. Alipowapa wanafunzi wake maagizo haya, ilikuwa ni muda mfupi tu kabla ya kwenda msalabani kisha

kuendelea kuwa na Baba mbinguni. Alitaka kuhakikisha wanafunzi wake wanajua kwamba uhusiano wao na yeye utaendelea, hata baada ya yeye kutokuwepo hapo kimwili.

**FAILI LENYE UKWELI**
*Kaa* -Kukaa, kubaki, kuendelea mahali, kuvumilia bila kujitoa.

**CHIMA ZAIDI**

Eleza tunapaswa kukaa wapi na matokeo yake ni nini.

> …Mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli.
> Nanyi mtaijua kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. (Yohana 8: 31-32)

______________________________________________________________________________

__________________________________________________

Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. (Yohana 15: 7)

Angalia jinsi Maandiko haya yanavyohusiana na kukaa kwetu ndani ya Kristo, kumtegemea yeye, na matokeo yake.

Sio kwamba twatosha sisi kufikiria neno lolote kwamba ni letu wenyewe, bali otoshelevu wetu unatoka kwa Mungu. (2 Wakorintho 3: 5)

Kwa hiyo hatulegei, bali ijapokuwa utu wetu nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani anafanywa upya siku kwa siku. (2 Wakorintho 4:16)

Maisha yetu ya ibada ni sawa na msingi wa nyumba. Huwezi kuuona, lakini nguvu yake inafunuliwa wakati dhoruba na majanga ya asili yanapotokea. Tunaweza kuwa na wasiwasi zaidi wa kutumia wakati wetu mwingi na pesa kuifanya nyumba ionekane nzuri, lakini msingi dhaifu unaweza kuleta hasara wakati wowote na kuifanya pesa iliyotumika kuwa bure. Ikiwa tutatumia wakati wetu kwenye picha tu ya mafanikio badala ya kukua katika haki, nyumba yetu itajengwa juu ya mchanga na itaanguka, kama vile Yesu alivyotabiri katika Mathayo 7. Ni msingi unaoshikilia nyumba, sio paa na rangi za kuvutia.

Katika masomo yafuatayo, utapata zana za kibiblia za kuwa na ndoa inayomcha Mungu. Lakini, ukiruka kanuni hii ya kiroho na kupuuza msingi wako, utarudi kwenye tabia zako za zamani. Kuendelea na mazoezi ya uhusiano wako na Mungu, katika Kristo, ndio msingi pekee ambao unaweza kujenga kwa ajili ya mafanikio.

**Uasi na Chaguzi**

Unaposikia neno *uasi*, ni nini kinakuja akilini? Vijana? Uasi mara nyingi huhusishwa na vijana. Lakini, uasi unamaanisha kupinga yoyote kwa mamlaka. [14] Baada ya kuchagua kufanya mambo kwa njia yako, ikiwa ni pamoja na kuweka vipaumbele kulingana na tamaa yako badala ya mafundisho ya Mungu, hiyo ni ya uasi. Kuchagua kutotenga wakati wa uhusiano wa karibu na Bwana ni uasi.

Kukuza urafiki na kukaa ndani ya Kristo ni chaguo, na Mungu anatuambia wazi katika Maandiko kufanya yote mawili. Aliwaambia Waisraeli katika Kumbukumbu la Torati 6, kabla ya kuingia katika nchi ya ahadi, wampende Mungu kwa moyo wao wote, akili, mwili na roho. Tunatumia wakati na watu tunaowapenda, na lazima tuchague kila siku kumpenda Mungu kwa kutumia muda kumjua yeye vizuri, kutafuta Biblia kwa ukweli wa kiroho, na kisha, kwa neema yake, kuijenga katika maisha yetu kwa njia ya sala na utii.

Mmomonyoko wa msingi wetu wa kiroho, uhusiano wetu na Mungu, huanza na kupuuza maisha yetu ya ibada na kawaida husababisha yafuatayo:

1. Tunaacha kujitolea na kuanza kuuliza, "Je! Mimi, hisia zangu, na mahitaji yangu vipi?"
2. Tunaanza kujifurahisha kwa kujionea huruma na kuonyesha upendo, badala ya masharti.
3. Tunaacha kukosa njaa na kiu ya (kutafuta) utakatifu.
4. Tunaanza kuhalalisha mitazamo yetu ya dhambi, tabia, na ubinafsi kwa wenzi wetu na wengine.
5. Tunaanza kulaumu wengine kwa shida zetu, mitazamo ya dhambi, na tabia zetu.

**Kujichunguza**

Je! Unaonyesha aina yoyote ya mawazo au tabia hizi? Orodhesha. Ungama kwa Bwana na uombe msamaha wake. Yohana wa Kwanza 1: 9 inasema, "Tukikiri dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atusamehe dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

Je! Tunawezaje kupambana na tabia yetu ya asili ya kupuuza, ambayo inasababisha kutojali na dhambi? Lazima tujizoeshe. Katika 1 Wakorintho 9:27, mtume Paulo aliandika, "Ninauadhibu mwili wangu na kuuweka chini ya mamlaka." Alielewa kuwa alihitaji kufanya kazi, kwamba alihitaji kufundisha mwili wake mwenyewe kuufanya ufanye kile ambacho kwa kawaida hakutaka kukifanya. Mara nyingi Paulo alitumia mifano ya riadha kutoa hoja yake. *Nidhamu* ni timu ya mchezo wa ngumu.

Je! Ni yapi mawazo yako ya kwanza asubuhi? Unapokuwa umelala kitandani na ukawa na fahamu, mawazo yako ya kwanza ni yapi? Jifunze kwa njia hii: kitu cha kwanza asubuhi, elekeza akili yako kwa Kristo, na ukumbuke au ujitambue mwenyewe kwa Mungu jinsi unavyohitaji nguvu yake kupigana na tamaa zako za asili za dhambi. Jambo kubwa ni kwamba Mungu tayari anajua mapambano yako. Wakati ulikuwa bado mwenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yako (Warumi 5: 8). Sasa, katika Kristo, Mungu anaweza kupitia: "Mimi hapa. Nataka kukubariki. Nakupenda."

**FAILI LENYE UKWELI**
*Nidhamu* - *Hupopiazo* (Kigiriki).
Inatumika kuelezea mabondia wanaotoa makofi ya mtoano, ngumi kwa sehemu ya uso chini ya macho, hadi walipokuwa weusi na bluu. Vifungu vinavyohusiana: 1 Timotheo 4: 7-8; Yuda 3; 2 Petro 1: 5-6.

**CHIMA ZAIDI**

Je! Maandiko haya yanatufundisha nini juu ya mawazo ya mtunga zaburi asubuhi? Alikuwa akifanya nini?
Unawezaje kujikumbusha kumfikiria Mungu kwanza, kabla ya kutoka kitandani?

> Bwana, asubuhi utaisikia sauti yangu.
> Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia. (Zaburi 5: 3)

> Kutangulia mapambazuko, naliomba msaada; naliyangojea maneno yako kwa tumaini. (Zaburi 119: 147)

Mungu anajua kila kitu. Anajua jinsi tunavyoweza kuwa dhaifu na wapumbavu na "taka" zote tulizokuwa nazo wakati alipotuchukua kama watoto wake. Alitujua na kutuchagua bila

kujali. Yeye hayuko hapa kutuhukumu, lakini anatamani kutubariki. Lazima tufundishe akili zetu. Unapoamka, acha kufanya mawazo yako ya kwanza, mawazo yako yawe,"Mungu mimi hapa. Asante kwamba mimi ni mmoja wako! Najua maeneo mengi katika maisha yangu yanahitaji kuboreshwa. Mungu, ninahitaji nguvu zako. ” Bwana anatamani kusikia ukisema hivyo kila siku.

Jifunze kujikita kwa Yesu katika nyakati za kwanza za asubuhi; sio kwenye bili yako, mwenzi wako, watoto wako, au kazi yako, bila kujali jinsi mambo haya yanavyoweza kuonekana. Omba, umwombe neema yake kuipenda familia yako na kutembea katika mapenzi yake, kabla ya kuanza shughuli zozote za siku hiyo.

> Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa chochote
> apandacho mtu, ndicho atakachovuna. (Wagalatia 6: 7)

Ikiwa tutamtanguliza Mungu mbele ya vitu vyote, tutavuna ahadi zote zinazotungojea katika yeye. Weka akili yako kwa Mungu, kisha uwe na wakati wako wa ibada, lakini pia lazima urudi kwake kwa njia ya mawazo wakati wa mchana. Lazima tumtegemee Mungu na kutii wakati tunakabiliwa na taabu, pamoja na shida katika ndoa zetu.

Angalia jinsi Mungu anavyotaka tupatanishe mawazo yetu.

> Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuta yale yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu.Yafikirini yaliyo juu siyo yaliyo katika nchi. (Wakolosai 3: 1-2)

Je! Mazoezi haya yanawezaje kusaidia wakati unapata shida katika ndoa yako?

**FAILI LENYE UKWELI**

*Tafuta na uweke akili yako* - Hivi vitenzi muhimu zinaonyesha kuwa kitendo ni mchakato wa kuendelea.

*Kutafuta*- kuangalia kwa kina kujitahidi kupata.

